Ijumaa Februari 2, 2024 • Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

# Nipashe

ISSN 0856 • No. 0581574
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII

LIKE & FOLLOW US
www.twitter.com/nipashetz
www.facebook.com/nipashetz
www.instagram.com/theguardian_newspaper



**NYOTA WA 5 WANAOWEZA KUTUA KLABU KUBWA ULAYA**

UKURASA 21

# Samia afunda majaji dhidi ya upendeleo



UKURASA 2



**MAANDAMANO** CHADEMA majiji matatu baada ya Dar es Salaam

UKURASA 3

**KINACHOSUBIRIWA** SGR kimekaribia kutoka ahadi ya Rais Samia 2021

UKURASA 11



**ZANZIBAR** kujenga ukuta kuzuia maji ya bahari kuvamia maeneo ya makazi

UKURASA 7

## WAZIRI KUJIUZULU

# Mwinyi avunja ukimya

**ATAJA** yaliyo nyuma ya pazia; afunguka uzoefu unaofanana akiwa Waziri wa JK... *Endelea ukurasa wa 2*



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi



Simai Mohamed Said







Baadhi ya wakazi wa kitongoji cha Mbalwa, kijiji cha Engikaret, wilayani Longido mkoani Arusha, wakitoa mabaki ya vitu vyao, baada ya makazi wanayoishi, maarufu maboma, kuchomwa moto na watu wasiojulikana juzi mchana. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Adaiwa kumchinja mkewe, kumpasua tumbo, atoa pacha



UKURASA 4

**MICHEZO** SIMBA WAWAGEUKIA MASHUJAA, TABORA UK. 23

**KATUNI** UK. 6




Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia maadhimisho ya Siku ya Sheria Kitaifa katika viwanja vya Chinangali, jijini Dodoma jana. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# Mwinyi avunja ukimya Waziri kujiuzulu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar Dk Hussein Ali Mwinyi amesema kitendo cha waziri kujiuzulu ni njia mojawapo ya uwajibikaji hasa pale inapotokea changamoto katika sekta anayoiongoza.

Wakati akibainisha hayo, Dk. Mwinyi ametoboa siri kwamba alitaka kujiuzulu kutokana na mabomu ya Gongo la Mboto lakini aliyekuwa Rais wa Awamu ya Nne, Dk. Jakaya Kikwete, alimgomea kwa kuwa ilikuwa ajali.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo jana baada ya kuwaapisha mawaziri na naibu mawaziri aliowateua hivi karibuni, katika viwanja vya Ikulu, Zanzibar. Rais alifanya mabadiliko madogo baada ya aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, kujiuzulu wadhifa huo.

Alisema suala la kujiuzulu si geni Zanzibar bali ni sehemu ya uwajibikaji na kuna maudhui mawili ya waziri kujiuzulu ikiwamo kutokea matatizo katika sekta anayoiongoza kwa sababu yeye ni msimamizi mkuu. Alitoa mfano wa Waziri mwenye dhamana ya uchukuzi alipojiuzulu baada ya meli ya Spice Island kuzama baharini na kusababisha vifo vya watu.

"Lilipotokea suala la aliyekuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Simai Mohamed Said, kujiuzulu nimekuwa nasikia katika mitandao kuwa Zanzibar hajawahi mtu kujiuzulu wadhifa wake.

Si kweli wakati wa ajali ya Meli ya MV Spice Island kuna waziri alijiuzulu kwa sababu ya kuwajibika kutokana na changamoto katika sekta aliyokuwa anaiongoza. Lakini ile ilikuwa kutokana na uzembe kwa sababu meli ilijaza kupita uwezo wake naye hakuchukua hatua," alisema Dk. Mwinyi.

Pia alisema Waziri anaweza kuchukua hatua ya kujiuzulu pindi linapotokea tatizo lakini si kwa kuanza kuzungumza na vyombo vya habari au kutoa taarifa kwenye mitandao bali kwa kuanza kuwasilisha barua kwa aliyemteua.

ATOBOA SIRI

Rais Mwinyi alitoa siri ambayo hajawahi kuisema kuhusu kusudio alilolitoa kutaka kujiuzulu alipokuwa Waziri wa Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa wakati wa serikali ya awamu ya nne ya Tanzania chini ya Rais Kikwete.

Alisema wakati wa tukio la mabomu ya Gongo la Mboto, alipeleka ujumbe kwa Rais Kikwete kutaka aridhie ajiuzulu, lakini hakukurupuka kwenda katika vyombo vya habari kutangaza kwamba amejiuzulu. Rais Kikwete alimkatalia kwa kuwa ilikuwa ajali ambayo hakuisababisha .

"Si utaratibu wa kukimbilia kwenye vyombo vya habari. Utaratibu unataka umwambie aliyekuteua akubali ndipo ukatangaze.. Leo (jana) ninasema hili hadharani na sijawahi kulisema," alibainisha.

Dk. Mwinyi alisisitiza kuwa kujiuzulu ni njia ya kuwajibika, hivyo aliwataka mawaziri ikiwa lazima kujiuzulu au kuwajibika ni vyema kufanya hivyo.

Alisema sababu nyingine ya waziri kujiuzulu ni pale serikali inaamua jambo na waziri hakubaliani nalo kwa mantiki hiyo, waziri ana haki ya kujiuzulu kwa sababu hakubaliani na uamuzi wa serikali.

"Lakini kuna jambo moja lazima tukumbushane wakati unawajibika kwa njia yoyote. Lazima uwe mkweli na ukweli ninaozungumzia hapa ni pale kama kuna mgongano wa maslahi, utangaze useme ukweli na kuwa muwazi kama tumezuia kitu na wewe una biashara hiyo, basi tangaza," alisema.

Dk. Mwinyi alisema lazima mawaziri kuwa wakweli kuliko kutoka kwenda katika mitandao na kuuaminisha umma na kwamba kinyume chake si sahihi na mtu anapojiuzulu lazima auambie umma sababu ya kuchukua uamuzi huo.

"Haya nayasema kwa sababu nataka mawaziri ambao mpo mtambue hilo maana uwaziri si nafasi ambayo utakaa nayo maisha. Kuna njia nyingi ambazo utatoka katika uwaziri ama utaondolewa au utawajibika kwa tatizo litakalotokea," alisisitiza.

Alitaka mawaziri hao kujua kuna matatizo yanaweza kutokea katika sekta wanazoziongoza na matatizo hayo si lazima wasababishe wao lakini wao ndio wasimamizi, hivyo wanapaswa kuwajibika na pale ambapo hakubaliani na serikali kusema na kuwa muwazi ataheshimiwa.

"Kama una baa watu wamezuia pombe, sema 'nina baa, inaingiliana na maslahi yangu', ni vyema kuwa muwazi," alisema.

Aliongeza kuwa mabadiliko katika baraza la mawaziri, si kitu cha ajabu katika siasa na wakati mwingine yanafanyika kwa ajili ya kuleta ufanisi na kuwataka mawaziri kufahamu kwamba nafasi hizo si za kudumu, hivyo kila mmoja afanye kazi kwa bidii ili kutimiza yale waliyowaahidi wananchi.

KAULI YA SIMAI

Simai jana alitoa taarifa kwa vyombo vya habari baada ya Rais Mwinyi kuzungumza akisema: Kiutamaduni si busara kuhoji, kujibu, kuongeza au kupunguza kauli ya Mheshimiwa Rais akitoa kwenye vyombo vya habari, labda ingekuwa ndani ya vikao vya Chama Cha Mapinduzi au Baraza la Mawaziri."

Hata hivyo, alisema aliteuliwa kuwa waziri kutumikia Wazanzibari katika sekta ya utalii, ambayo inabeba zaidi ya asilimia 75 ya uchumi wa Zanzibar. Kutokana na hali hiyo, alisema sekta hiyo ni uhai wa Zanzibar na ni eneo nyeti.

Simai aliweka bayana kuwa Rais Mwinyi amesisitiza kuhusu kusema kweli wakati wa kujiuzulu, jambo ambalo amelifanya na alimpatia barua ya kujiuzulu.

Kuhusu kukimbilia kwenye vyombo vya habari, alisema kuna umuhimu wake na kwamba baada ya kuandika barua kwa Rais kuhusu kujiuzulu, ni vyema pia kuujulisha umma.

"Waziri ni mtumishi wa umma, hivyo basi Mheshimiwa Rais yuko sahihi na ndicho nilichofanya, kuandika barua na kisha kuujulisha umma," alisema.

# Samia awafunda majaji utoaji haki

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewataka Majaji na Mahakimu kutoa hukumu kwa kuzingatia haki ili kukomesha malalamiko ya wananchi kutumikia adhabu ambazo hawastahili.

Alisema hayo jana jijini hapa alipokuwa akizungumza kwenye kilele cha maadhimisho ya Wiki ya Sheria na mwaka mpya wa kuanza kwa shughuli za mahakama.

"Kutoa haki ni kazi ya Mungu. Ukitoa kwa dhuluma umetenda dhambi na dhambi ni aibu kwa mujibu wa vitabu vitakatifu. Ni aibu pale ambapo wewe utatoa hukumu ya dhuluma lakini familia ya yule ambaye umemfunga kwa dhuluma itaendelea kupata shida mtaani, hivyo jiepusheni na hukumu zenye dhuluma.

"Mheshimiwa Jaji Mkuu, Ibara ya 107(a) kifungu kidogo cha pili (a) mpaka e cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, imeweka kanuni za kuzingatiwa pindi mahakama inapotoa uamuzi wa mashauri mbalimbali. Kanuni hizo ni kutenda haki kwa wote bila kujali hali ya mtu kijamii na kiuchumi," alisema.

Pia alisema kifungu hicho kimeelekeza kutocheleweshaa haki bila sababu ya msingi, kukuza na kuendeleza usuluhishi baina ya wanaohusika katika migogoro na kutenda haki bila kufungwa kupitia kiasi au kasi ya masharti ya kiufundi ambayo yanaweza kukwamisha kutenda haki.

Kadhalika Rais aliwataka wadau wote wa utoaji haki nchini kujitathmini na kubaini kasoro zao na kuzifanyia kazi ili kuboresha eneo hilo la utoaji haki.

"Jitihada kubwa zimefanyika hasa katika eneo la haki jinai, hivyo iko haja ya kuongeza jitihada katika eneo la haki madai na kwenyewe pia kuna malalamiko. Kesi zinacheleweshwa mzunguko ni mkubwa. Wanasema inachukua hadi miezi 12 kwa shauri lililoko mahakama ya wilaya na mahakama ya hakimu mkazi kusikilizwa hadi kuhitimishwa.

"Na kwa upande wa Mahakama Kuu, inachukua hadi miezi 24 kwa shauri kusikilizwa hadi kutolewa hukumu. Sasa hii inachukua muda mwingi wa wadau wanaohusika kwenye mashauri haya na wanapoteza muda mwingi wa kufanya mambo mengine muhimu kwa jamii. Niombe sana na huko nako kutupiwe macho," alisema.

Rais pia aliwataka wadau wa utoaji haki nchini kuharakisha maamuzi kwenye kesi za kibiashara na migogoro ili ziishe haraka na mambo mengine kuendelea.

"Tunatambua kwamba uwekezaji huambatana na masuala ya kisheria hivyo migogoro ya kibiashara ni vyema mahakama zetu kutoa umuhimu wa mashauri ya aina hiyo pia," alisema na kusisitiza kwamba kuna haja ya kuangalia namna bora ya kuanza kutumia usuluhishi katika mashauri badala ya watu kwenda mahakamani.

Kutokana na hali hiyo, aliiagiza Wizara ya Katiba na Sheria kushirikiana na wadau wa usuluhishi kusaidia kuudwa kwa sera ya masuala yanayohusu usuluhishi.

Kuhusu kampeni ya msaada wa kisheria ya Mama Samia Legal Aid, alisema imepokewa vizuri na wananchi ambao walikuwa na uhitaji mkubwa wa masuala ya kisheria.

"Kwa jinsi ilivyopokewa kampeni hii, ni wazi kuwa kuna uhitaji mkubwa sana wa kisheria hapa nchini. Tayari kampeni hiyo imewafikia watu 383,293 katika mikoa ya Dodoma, Shinyanga, Singida, Manyara, Ruvuma na Simiyu na migogoro takribani 511 ilitatuliwa," alisema.

Alisema kampeni hiyo imeisaidia serikali kubaini maeneo ambayo yana migogoro mingi zaidi kwenye jamii yakiwamo ardhi, ndoa, mirathi, ukatili wa kijinsia na madai.

Jaji Mkuu wa Tanzania, Prof. Ibrahim Juma, alisema wakati wa kulaumiana umepita na sasa ni utekelezaji na mahakama inaahidi kuwa mstari wa mbele kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

"Ushirikiano baina ya taasisi za hakijinai ni jambo muhimu sana kwa mfano mahakama tumepiga hatua kubwa katika maboresho kitengo chetu cha maboresho kiko tayari kuwasaidia wadau ambao wanataka kujifunza maboresho. Kitengo chetu cha TEHAMA (Teknolojia ya Habari na Mawasiliano) kimejijengea uwezo mkubwa wa kutengeneza mifumo inayokidhi mahitaji ya Tanzania.

"Kama mnataka kufanya maboresho njooni katika vitengo hivi vitawapa elimu ndiyo maana majaji wakuu kutoka Zimbabwe, Uganda kila mara wanatuma watu kuja kujifunza kwetu," alisema.

HABARI KITAIFA

# CHADEMA yatangaza awamu ya pili maandamano majiji matatu

**Na Jenifer Gilla**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), kimetangaza awamu ya pili ya maandamano ya kuishinikiza serikali kutekeleza maagizo yaliyotolewa awamu ya kwanza, yatakayofanyika katika majiji ya Mwanza, Mbeya na Arusha.

Maandamano hayo ni mwendelezo wa yaliyofanywa Januari 24, mwaka huu, jiji la Dar es Salaam yenye lengo la kuishinikiza serikali kuondoa bungeni miswada mitatu ya mabadiliko ya sheria za uchaguzi, kuboresha Katiba na kuwapunguzia wananchi mzigo wa hali ngumu ya maisha.

Akizungumza na waandishi wa habari jana, Katibu Mkuu wa CHADEMA, John Mnyika, alisema wanaendelea na maandamano hayo baada ya serikali kutofanyia kazi matakwa yao walioyapeleka katika ofisi za Umoja wa Mataifa katika maandamano ya kwanza.

Alisema CHADEMA ilitarajia kuwa baada ya maandamano yaliyofanyika jijini Dar es Salaam hadi katika ofisi za Umoja wa Mataifa na kuwasilisha barua yenye matakwa hayo, serikali ingesikiliza wananchi.

Alisema badala yake iliendelea kuisoma miswada hiyo kwa mara ya pili bungeni Januari 30, mwaka huu na wabunge kuijadili jambo aliloiita kuwa ni kupuuza maoni na matakwa ya wananchi.

"Mosi serikali ingeondoa miswada mibovu bungeni, pili ingetoa kauli ya kuwasilisha mpango maalum wa makusudi wa dharura wa kupunguza ugumu wa maisha kwa wananchi," alisema.

Mnyika alisema hatua pekee waliyoiona kuchukuliwa na serikali ni kutangaza bei elekezi ya sukari bila ya kuchukua hatua za msingi za kudhibiti ongezeko kubwa la bei la bidhaa hiyo nchini.

"Matatizo ya msingi yanayochangia ugumu wa maisha ikiwamo ukubwa wa mgawo wa umeme katika taifa letu yameendelea kutamalaki bila kuchukuliwa hatua na serikali," alisema.

Alisema maandamano hayo yataanzia katika Jiji la Mwanza Februari 13, mwaka huu, litafuata Mbeya Februari 20 na kufuatiwa na Arusha Februari 27 na kwamba wameshafanya mawasiliano na ofisi za kanda za chama hicho kwa ajili ya kuanza kufanya maandalizi.

Kadhalika, baada ya maandalizi kufanyika watautaarifu umma njia za kupita na masuala mengine yahusuyo maandamano hayo.

Alisema baada ya maandamano hayo kufanyika wataeleza hatua zaidi za kuchukua ili kuendelea kuishinikiza serikali kuheshimu maoni na kutekeleza matakwa yao kama walivyoyaainisha.

"Tutaendelea na maandamano ya kuiwajibisha serikali, kuitaka ichukue hatua katika masuala ya msingi yanayowagusa wananchi na nchi," alisema.

Aidha, Mnyika aliwakumbusha wadau wa sheria hasa mahakama wakati wanasherehekea siku ya sheria duniani kuikumbuka ibara ya 107a ya Katiba ya nchi kwa kusimamia haki kwa kuwa imekuwa ikisita katika kutimiza wajibu wake huo wa msingi mpaka mahakama za juu za kikanda zinaamua kuingilia kati.

Alizikumbusha mahakama nchini kujifunza kutoka kwenye hukumu ya mahakama ya Afrika Mashariki iliyochambua sheria ya vyama vya siasa ya nchi hiyo na kuainisha vifungu ambavyo vilistahili kubadilishwa, lakini bado haitekelezi agizo hilo.

Alitoa pia wito kwa mawakili wote nchini kuwa wakati CHADEMA ikiendelea kuwaongoza wananchi kupitia maandamano kupata haki walizoziainisha, kuzitumia mahakama kuendesha mapambano kusimamia haki hiyo.

Aliwashukuru wadau wote wa haki kutoka taasisi mbalimbali nchini waliojitokeza na kuwaunga mkono katika maandamano ya kwanza na kutoa wito kwa wadau wengine na wananchi katika majiji yatakayofanyika maandamano kuungana nao kudai haki zao za msingi.

## Rais aongeza fungu kutibu watoto wanaougua sikoseli

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

RAIS Samia Suluhu Hassan ametoa nyongeza ya Sh. bilioni moja kwa ajili ya kusaidia upandikizaji uloto kwa watoto 13 wenye ugonjwa wa selimundu walioko katika Hospitali ya Benjamin Mkapa, mkoani Dodoma.

Jana Rais Samia alitembelea hospitali hiyo na kujulia hali wagonjwa mbalimbali, wakiwamo watoto waliopona ugonjwa wa selimundu.

Akiwa hospitalini huko, Rais Samia alihimiza wazazi wa watoto hao kutunza watoto wao ili afya zao ziimarike kwa kuwa matibabu yao ni ya gharama kubwa.

"Ninyi peke yenu isingewezekana, ndiyo maana serikali imebeba jukumu, tukisikia wameumwa roho zinatuuma. Kwahiyo, mjitahidi kuwatunza," aliagiza Rais Samia.

Waziri wa Afya, Ummy Mwalimu alisema kuwa awali serikali ilitoa fedha za kugharamia matibabu ya watoto saba waliokuwa wanahitaji huduma ya upandikizaji uloto.

"Leo (jana) Rais Samia ameongeza fedha hizo ili kufikia idadi ya watoto 20 hadi Juni 2024," alisema Waziri Ummy.

Mwanzoni mwa juma hili, hospitali hiyo ilitangaza kuwa watoto watatu wamepona ugonjwa wa selimundu baada ya kuwafanyia matibabu ya upandikizaji uloto.

Mkurugenzi Mtendaji wa Hospitali hiyo, Dk. Alphonce Chandika alitangaza mafanikio hayo Jumanne ya juma hili ikiwa ni mwaka mmoja tangu hospitali hiyo ifanye matibabu ya upandikizaji wa uloto kumtibu mtoto mwenye ugonjwa wa selimundu (sikoseli).

Dk. Chandika alisema watoto hao hawana maradhi ya selimundu tena. Serikali chini ya uongozi wa Rais Dk. Samia Suluhu Hassan imewekeza zaidi ya billioni 3.6 kuwezesha huduma hizo ili kuokoa maisha watanzania.

Watoto hao ni Grace Hosea (8), Elisha John (11), na Isack Kedmond (10). Matibabu ya upandikizaji uloto yanagharimu kati ya Sh milioni 55 na milioni 65.



# Adaiwa kumchinja mkewe mjamzito, kupasua tumbo kutoa watoto pacha

**Na Halima Ikunji,** TABORA

HAMISI Kulwa (35), mkazi wa Kata ya Uyogo, wilayani Urambo, mkoani Tabora, anashikiliwa na Jeshi la Polisi kwa tuhuma za kumchinja mke wake mjamzito na kumpasua tumbo kutoa watoto pacha kisha kumpika mmoja wao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Tabora, Kamishna Msaidizi wa Polisi Richard Abwao, alisema jana ukatili huo ulifanywa Januari 30, mwaka huu saa 11 jioni katika Kitongoji cha Isunda, Kijiji cha Milambo, ukihusishwa na imani za kishirikina.

Alisema mtuhumiwa huyo alitekeleza ukatili huo kwa mkewe kwa kumchinja kisha watoto wake watatu (pacha wawili waliokuwa tumboni na mwingine aliyekuwa na umri wa miaka miwili) kuwazika huku akiupika mwili wa mmoja wa pacha aliowatoa tumboni mwa mkewe baada ya kumpasua kienyeji.

Kamanda Abwao alisema tukio hilo linahusishwa na imani za kishirikina kwa kuwa mwanamume huyo alipokamatwa na kuhojiwa alidai mke na watoto walitakiwa kupelekwa 'Gambushi' (eneo lililoko mkoani Simiyu linaloaminika kwa nguvu za giza.

"Wakati wa mahojiano alidai kuwa aliambiwa kuna watu wametumwa kumchukua mkewe na watoto, wanawapeleka Gambushi kufanya kazi za kichawi usiku na siku si nyingi wangewachukua na kuwaua ndio maana akaamua awaue yeye mwenyewe," alisema Kamanda Abwao.

Alisema jeshi hilo linaendelea na upelelezi, ukikamilika watamfikisha mtuhumiwa huyo mahakamani kwa mujibu wa sheria ili kujibu tuhuma hizo za mauaji.

**MAUAJI SHINYANGA**

Katika hatua nyingine, mkoani Shinyanga kumeripotiwa tukio la Rebeca Machiya (36), mkazi wa Mtaa wa Mwasele 'B', Kata ya Kishapu, wilayani humo aliyekutwa amefariki dunia ndani ya chumba chake, huku akiwa amenyofolewa macho, matiti na sehemu za siri.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya hiyo Joseph Mkude, Jeshi la Polisi lilibaini kufanywa ukatili huo Januari 30, mwaka huu, ukihusishwa na imani za kishirikina. Aliwataka waganga wote wa jadi wilayani Kishapu kufanya uchunguzi wa haraka ili kuhakikisha viungo hivyo vimepatikana na wahalifu wanatiwa mbaroni.

"Nimeona niwaite waganga wote wa jadi ili kuwashirikisha suala hili, kwani kifo cha mama huyu ni cha aibu sana. Niwaombe tushirikiane kwa pamoja ili viungo vya huyu mama vipatikane, kuna watu wanafikiri kufanya hivyo ni kutajirika, huwezi kutajirika kwa kunyofoa viungo vya binadamu. Niwaombe mtoe ushirikiano wa haraka," aliagiza Mkude.

Mkuu wa Wilaya pia aliwaomba viongozi wa dini waendelee kuhubiri ili kudumisha amani, huku akiagiza madiwani waendelee kukemea jambo hilo ili lisijitokeze tena katika wilaya hiyo na maeneo mengine.

Mwenyekiti wa Waganga wa Tiba Asili Wilaya ya Kishapu, Ndembi Mabeshi alisema walifanya kitendo hicho ni watu ambao wana maslahi yao. Si waganga wa jadi. Waliahidi kusaidia uchunguzi kuwabaini wahusika.




Mkuu wa Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE), Prof. Edda Lwoga (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, kuhusu chuo hicho kuanzisha kozi za Shahada za Umahiri mtandaoni (online masters degree) kwa fani sita. Kushoto ni Mkurugenzi wa Taaluma wa chuo hicho, Dk. Shima na Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Taaluma, Utafiti na Ushauri, Dk. William Gomera. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Serikali kukamilisha mpango wa uendelezaji ufugaji nyuki

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI ipo mbioni kukamilisha mpango wa kuendeleza sekta ya ufugaji nyuki ambao utachochea uzalishaji, mauzo ya asali nje ya nchi pamoja na ajira hasa kwa vijana na wanawake.

Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, Dastan Kitandula, alibainisha hayo jana jijini hapa alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Tabora Kaskazini (CCM), Almas Maige.

Mbunge huyo alihoji serikali ina mpango gani wa kufanya asali kuwa moja ya zao la kimkakati.

Naibu Waziri Kitandula alisema ufugaji nyuki ni moja ya shughuli muhimu za kijamii, kiuchumi na kiutamaduni kwa makabila mengi nchini hususani kwa jamii inayoishi kando kando na maeneo yaliyohifadhiwa kwa Afrika na katika maeneo mengi duniani.

Aidha, alisema ufugaji nyuki una mchango mkubwa katika kuhakikisha usalama wa chakula kupitia uchavushaji.

Alisema kuwa kwa kutambua umuhimu wa shughuli hiyo, serikali imechukua hatua kadhaa za kufanya asali kuwa zao la kimkakati.

Alitaja hatua hizo ni pamoja na kuimarisha mifumo ya usimamizi pamoja na kutoa miongozo mbalimbali inayohusu ufugaji nyuki; kuwezesha wafugaji nyuki kwa kuwapatia mizinga ya kisasa.

"Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita zaidi ya mizinga ya kisasa 64,593 imetolewa kwa vikundi vya wafugaji nyuki kutoka katika mikoa mbalimbali," alisema.

Alisema serikali imewezesha ujenzi wa viwanda saba vya kuchakata na kufungasha asali katika Wilaya za Sikonge, Mlele, Nzega, Tabora, Manyoni, Kibondo na Bukombe vitakavyotumika kuongezea thamani asali inayozalishwa na kuuzwa katika masoko ya ndani na nje ya nchi.

Kadhalika, serikali inatekeleza programu na miradi mbalimbali ya kuwezesha kuongeza uzalishaji wa asali na kutafuta masoko mapya katika nchi za Umoja wa Ulaya na Asia.

"Serikali kwa kushirikiana na wadau wa maendeleo inatekeleza mradi wa kuwezesha ufugaji nyuki katika mikoa mitano (Tabora, Singida, Katavi, Kigoma na Shinyanga) kwa upande wa Tanzania Bara na

## Waziri January azinadi Italia fursa za uwekezaji Tanzania

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, January Makamba, amenadi fursa za biashara na uwekezaji zinazopatikana nchini katika mkutano wa wafanyabiashara, viongozi wa siasa na wa kijamii huko Italia.

Waziri January amewaeleza wafanyabiashara na wawekezaji wa Italia fursa mbalimbali za biashara zinazopatikana nchini pamoja na mageuzi makubwa ya kuboresha mazingira ya uwekezaji yanayofanyika chini ya Rais Dk. Samia Suluhu Hassan.

Alisema mazingira ya biashara na uwekezaji nchini ni salama na rafiki kutokana na juhudi zinazofanywa na serikali ili kuhakikisha wafanyabiashara wanatekeleza majukumu yao.

Alisema Tanzania inazingatia misingi ya utawala bora pamoja na kuzungukwa na nchi saba ambazo hazina bandari na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na huduma kwenda katika nchi hizo. Pia alisema mazingira ya biashara na uwekezaji ya Tanzania ni salama kwa sababu imeridhia sheria na mikataba ya kimataifa inayolinda mitaji na uwekezaji wa kigeni pamoja na serikali kutambua sekta binafsi kama injini ya maendeleo kiuchumi. "Napenda kuwasihi wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Italia kuja kuwekeza Tanzania kwani licha ya kuwa na mzingira salama, pia kuna fursa za kuwekeza katika sekta mbalimbali kama nishati, utalii, kilimo, afya na elimu," alisema January.

Alisema Tanzania ni mwanachama wa Eneo Huru la Biashara barani Afrika (AfCFTA) ambalo linahusisha watu zaidi ya bilioni 1.5, itawezesha wafanyabiashara wa Italia kuwafikia watu hao kupitia soko hilo.

Alisema Tanzania iko tayari kushirikiana na Italia katika kutekeleza Mpango wa Mattei kwa maslahi ya pande zote mbili na kuwasisitiza kuchangamkia fursa za biashara na uwekezaji nchini Tanzania na visiwani Zanzibar.

Rais wa Chama cha Wafanyabiashara wa Italia, Alfredo Cestari, alisema utekelezaji wa mpango wa Mattei utakapoanza utazingatia maoni na mapendekezo yote yaliyotolewa na wadau na miradi ya kipaumbele kwa nchi nane za awali za Afrika ikiwamo Tanzania.

Tanzania ni moja kati ya nchi nane za Afrika zitakazopewa kipaumbele na Italia kupitia mpango mpya wa kimkakati wa Mattei (Mattei Plan) na Euro bilioni tano za awali zimetengwa kwa ajili ya utekelezaji wa miradi hiyo.

# Waziri Mkuu: Marufuku michango holela shuleni

**Na Godfrey Mushi,** DODOMA



WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa (pichani) kwa mara nyingine amesisitiza msimamo wa serikali kuhusu marufuku ya michango holela ya fedha kwenye shule za umma.

Wakati wa kipindi cha 'Maswali kwa Waziri Mkuu' bungeni jijini hapa jana, Majaliwa alisema msimamo wa serikali umebaki vilevile - michango holela hairuhusiwi.

Akijibu swali la Mbunge wa Korogwe Vijijini, Timotheo Mnzava, Waziri Mkuu alisema: "Msimamo wa serikali umebaki vilevile, kwamba michango holela hairuhusiwi. Ninaposema michango holela, tunajua tuna michango kidogo inakubalika kwenye jamii.

"Hizi shule zetu za msingi na sekondari, ni shule za jamii, ziko kwenye maeneo hayo na tumeunda kamati ya shule ya msingi, lakini tuna bodi ya shule za sekondari.

"Na wajumbe wa kamati na bodi hizi, ni wale walioko kwenye maeneo yale, ndio wanaopaswa kusimamia maendeleo ya shule, kushauri mwenendo wa shule, lakini pia kupata changamoto zinazotokana na mwenendo wa kila siku; na huwa wanashiriki katika usimamizi na uendelezaji shule hiyo na taaluma yake kwa ujumla.

"Kwa maana hiyo, kamati ya shule inajua inawajibika kwenye ile shule kufuatilia maendeleo yake lakini pia mahitaji yake. Inaweza kukatokea kwa mfano, choo kimebomoka cha Sh. milioni mbili. Si lazima kusubiri serikali ije kujenga choo.

"Jamii inaweza ikaweka mpango mkakati wa kujenga choo. Kwahiyo, michango holela na michango inayokubalika hapa iko ya aina mbili."

Majaliwa alisema iko michango inayokubalika ambayo ni ya maendeleo. Kamati ya shule hukutana na kuamua kwa haraka kutatua jambo la dharura.

Kuhusu udahili wa wanafunzi wa elimu ya awali, msingi na sekondari, Waziri Mkuu alilieleza Bunge kuwa hadi kufikia tarehe Januari 26, mwaka huu, idadi ya wanafunzi wa darasa la awali walioandikishwa ni 1,268,917.

Kati yao, wavulana ni 642,979 na wasichana ni 625,938 pamoja na wanafunzi wenye mahitaji maalum 2,366 wakiwamo wavulana 1,244 na wasichana 1,122.

Alisema wanafunzi waliondikishwa darasa la kwanza ni 1,549,743 wakiwamo wavulana 772,019 na wasichana 777,724 pamoja na wenye mahitaji maalum 3,311 wakiwamo wavulana 1,781 na wasichana 1,530.

Wanafunzi hao wa darasa la kwanza waliondikishwa, ni sawa na asilimia 89.6 ya maoteo ya uandikishaji wanafunzi 1,729,180 wenye umri wa miaka saba.

Kwa upande wa udahili wa wanafunzi wa kidato cha kwanza, Waziri Mkuu alisema udahili wao wanafunzi wa kidato cha kwanza unaendelea.

Majaliwa pia aliarifu Bunge kuwa serikali imekamilisha maandalizi ya Mfumo wa Tuzo wa Taifa (National Qualification Framework).

# Serikali yakiri mkanganyiko minada korosho kuathiri bei

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI imekiri kutambua kuwapo mkanganyiko wa minada ya korosho na masoko ya awali na kuathiri bei ya zao hilo kwa wakulima.

Naibu Waziri wa Kilimo, David Silinde, alibainisha hayo jana bungeni alipokuwa akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nanyamba (CCM), Abdallah Chikota.

Chikota alihoji kauli ya serikali kuhusu mwingiliano huo ili kumnusuru mkulima na anguko la bei ya zao hilo.

Akijibu, Silinde alisema kutokana na hali hiyo, Wizara ya Kilimo imeandaa mkutano wa wadau wa korosho kupitia mchakato na kwamba mfumo uliopo sasa hautakuwapo baada ya mkutano huo wa tathmini ya mkanganyiko huo.

Awali, katika swali la msingi, Mbunge wa Tandahimba (CCM), Katani Katani, alitaka kujua kama serikali ipo tayari kupunguza baadhi ya tozo kwenye zao la korosho ili kumsaidia mkulima kupata bei nzuri.

Silinde alijibu kuwa serikali inafanya maboresho ya kodi, ada na tozo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2015 na kuweka mazingira wezeshi ya biashara na uwekezaji kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji wa mazao ya kilimo ikiwamo zao la korosho.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha miaka minane (2015-2023), imefanya maboresho kwa kufuta tozo na ada 105 zilizokuwa zinatozwa kupitia Bodi na taasisi zilizo chini ya Wizara ya Kilimo.

"Katika kipindi cha miaka minane serikali imefanikiwa kufuta tozo sita katika zao la korosho ambazo zilionekana ni kero kwa wakulima," alisema.

Alisema huo ni utekelezaji wa mpango wa kuboresha mfumo wa udhibiti/usimamizi wa biashara.

"Katika kuimarisha na kuongeza uwekezaji katika sekta ya kilimo pamoja na kupunguza gharama kwa wakulima nchini, serikali itaendelea kufanya maboresho ya kodi, ada, tozo na ushuru kwenye mazao ya kilimo mazao ikiwamo zao la korosho ili kupunguza gharama za uzalishaji na kuongeza mapato kwa mkulima," alisema.


## JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
## WIZARA YA FEDHA

## MWALIKO KWA WADAU WA KUSHIRIKI KATIKA SHUGHULI ZA KAMATI YA MABORESHO YA SERA ZA KODI (TASK FORCE ON TAX REFORMS) KWA AJILI YA MATAYARISHO YA BAJETI YA 2024/25

Kamati ya Maboresho ya Sera za Kodi (Task Force on Tax Reforms) inayohusika na matayarisho ya Bajeti ya Serikali 2024/25 itaanza kazi yake mnamo mwezi Februari 2024. Vikao kazi vya Kamati vitazinduliwa na Kongamano la Kodi na Uwekezaji Kitaifa kwa mwaka 2024 ambalo litafanyika mwezi Februari.

Kila mwaka, Kamati hii, imekuwa ikipokea maoni ya wadau, kufanya uchambuzi, na kufanikisha majadiliano ya masuala mbalimbali yanayohusiana na sera za kodi na usimamizi wake. Maoni hayo yamekuwa na mchango mkubwa kwa waandaa sera na yamesaidia katika kuunda mfumo wa kodi ambao umewezesha utatuzi wa masuala mbalimbali ya kodi kwa ufasaha na uwazi.

Maboresho ya Sera za Kodi yanalenga kuboresha mazingira ya kufanya biashara ili kuvutia uwekezaji; kuwezesha ukuaji wa biashara ndogondogo na za kati pamoja na ukuaji wa uchumi endelevu; kuboresha mazingira ya ulipaji kodi wa hiari; upanuzi wa wigo wa kodi na matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika usimamizi wa kodi; kuimarisha usimamizi wa sheria za kodi ili kutatua changamoto za ukwepaji kodi, kupunguza upotevu wa mapato, kuwianisha na kupunguza tozo na ada mbalimbali ili kuboresha mazingira ya kufanya biashara na uwekezaji.

Ili kufanikisha suala hilo, Kamati inakaribisha ushiriki wa Taasisi za Serikali, Sekta Binafsi, Asasi zisizo za Serikali, Taasisi za Dini, Jamii ya Wasomi, Taasisi za Utafiti na Wataalamu wengine katika sekta ya uchumi kwa kutoa maoni ya kuboresha Sera za Kodi kwa maandishi. Vilevile, Kamati inakaribisha mada mbalimbali kutoka kwa wadau wanaopenda kufanya hivyo. Maoni na mada hizo zinapaswa kuonesha yafuatayo:-

i. Biashara, kampuni, taasisi, chama/vyama au makundi ambayo wanawakilisha;
ii. Mapendekezo ya mabadiliko ya kisera na mapato ya serikali yanayotokana na kodi na yasiyo ya kodi, ikiwa ni pamoja na uchambuzi wa sekta, maeneo au aina ya walipakodi ambao wataathirika, na kwa namna watakavyoathirika;
iii. Makisio ya athari kwenye uchumi na mapato ya serikali katika mwaka huu wa utekelezaji na katika miaka ijayo;
iv. Sababu na uhalali wa mapendekezo ya mabadiliko kwenye sera za mapato, hususan uchambuzi wa namna ambavyo mapendekezo hayo yataisaidia Serikali kufanikisha malengo yake makuu ya kiuchumi, kodi na kupunguza umasikini; na
v. Pale ambapo mapendekezo yanapunguza mapato ya Serikali (hata katika kipindi cha muda mfupi), mapendekezo hayo hayana budi yaweke hatua bayana na za kuaminika sambamba na msukumo wa jumla wa sera za bajeti ya Serikali ili kufidia upungufu wa mapato ambao utajitokeza.

Tunatarajia kupata mapendekezo yatakayowezesha majadiliano yenye tija kati ya Serikali na Wadau.

Mapendekezo yawasilishwe kuanzia tarehe ya tangazo hili hadi tarehe 31 Machi 2024 kupitia lango (portal) lifuatalo: **https://maoni.mof.go.tz/**

**Kwa Nakala Ngumu tafadhali wasilisha kwa anuani ifuatayo:**
**Sekretariati ya Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi,**
**Wizara ya Fedha na Mipango,**
**Idara ya Uchambuzi wa Sera,**
**Jengo la Hazina (Ghorofa ya Pili),**
**18 Barabara ya Jakaya Kikwete,**
**S.L.P 2802,**
**DODOMA.**

Barua Pepe: mathias.kadebe@hazina.go.tz au salha.mzee@hazina.go.tz

Kwa maelezo zaidi wasiliana na Mathias Kadebe **0713 694 895; au Salha Mzee 0652 442 944.**
Pia tembelea tovuti yetu: **www.mof.go.tz.**

**Tangazo hili limetolewa na:**

**Dkt. Natu E. Mwamba**
**Februari 2024**

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Viongozi, watendaji watambue wajibu kwa nafasi walizopewa

**MALALAMIKO** ya wananchi kuhusu kutokutendewa haki au kukosa huduma muhimu katika maeneo mbalimbali yamekuwa yakijitokeza siku hadi siku ilhali wako viongozi waliopewa dhamana.

Licha ya kutokupata haki na huduma, pia wananchi wamekuwa wakidai kunyanyaswa na viongozi na watendaji waliopewa dhamana ya kuwaongoza katika maeneo hayo.

Jambo hili limekuwa sugu kutokana na kuwapo kila mara huku wananchi wakilalamika.

Taarifa mbalimbali zimetolewa kuhusu matatizo hayo ikiwamo viongozi kuwapora wananchi mali zao au kuwakandamiza kwa kuwakumbatia matajiri kwenye mogogoro mbalimbali ikiwamo ya ardhi na mali.

Hayo yamejitokeza katika ziara mbalimbali za viongozi wakuu wa serikali, wakiwamo Rais, Makamu wa Rais na Waziri Mkuu Pamoja na viongozi wakuu wa chama tawala - Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Katika ziara hizo, wananchi wamekuwa wakiwapokea viongozi hao kwa mabango yanayowalalamikia viongozi wa maeneo husika hasa mikoa na wilaya kushindwa kutatua kero zao na kwa kiasi kikubwa kuwa sehemu ya kuwandandamiza na kuwanyang'anya mali zao.

Wakati za uongozi wa serikali ya awamu ya tano, chini ya Hayati Dk. John Magufuli, hali ya viongozi kupokewa kwa mabango ilishamiri kiasi cha kiongozi huyo kuwatumbua baadhi ya viongozi kwa kushindwa kutekeleza wajibu wao katika kuwahudumia wananchi.

Walijiona kuwa na nafasi hizo ni sehemu ya kujipatia mali kwa njia isiyo halali na hata kuwa miungu watu.

Hata Rais Samia Suluhu Hassan alipoingia madarakani baada ya kifo cha Magufulu, hali hiyo iliendelea kwa kupokewa na mabango. Hatua hiyo ilimfanya afikie uamuzi wa kusema amechoka na tabia hiyo, hivyo ikitokea kiongozi anayehusika atawajibishwa.

Pamoja na kukatazwa kwa mabango hayo, ziara ya Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC) ya CCM, Uenezi, Itikadi na Mafunzo, Paul Makonda, inayoendelea sasa katika mikoa mbalimbali, jambo hilo limeendelea kwa kuibuliwa kero mbalimbali kutoka kwa wananchi.

Baadhi ya wananchi wanaeleza kwamba wameporwa mali zao, ikiwamo ardhi na kwamba wanapokwenda katika vyombo huusika kama vile polisi, hawatendewi haki.

Baadhi ya wananchi hao wamefika mbali zaidi kwa kudai kuwa miongoni mwa watu wanaohusika kuwapora mali zao ni askari polisi waliopewa dhamana ya kindanda usalama wa raia na mali zao.

Mfano ni katika mkoa wa Shinyanga ilipoelezwa kuwa askari polisi alishirikiana na mfanyabiashara kupora fedha na mali za mwanamke anayemiliki mgodi.

Mbaya zaidi, hata Kamanda wa Polisi wa Mkoa amedaiwa kuwa alipofikishiwa, hajachukua hatua zinazostahili.

Ni vyema viongozi, watumishi na watendaji katika ngazi mbalimbali serikalini wakatambua kwamba nafasi walizopewa ni dhamana kwa ajili ya kuwatumikia wananchi.

Kwa maneno mengine wako katika nafasi hizo si kwa manufaa binafsi bali kuwatumikia wananchi kwa kutatua kero zinazopowakabili.

Ziara ya Makonda katika mikoa 10 inayoendelea sasa, iwakumbushe viongozi na watendaji hao Pamoja na kuwaamsha usingizini kama walishajisahau katika kutekeleza majukumu yao kwa kufuata sheria, kanuni, taratuibu na miongozo.

Wanaopaswa kubadilika na kurejea kwenye mstari wa kutelekeza kazi zao kama ilivyoainishwa katika miongozo yao.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Dennis Ntaita, 0713 578 284
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Kuna shida tunavyotumia mitandao jamii, turudie darasa lake kujifunza

Na Christina Mwakangale

**KILA** uchao, mitandao ya kijamii imekuwa ikipigiwa kelele duniani kuwa imekuwa ikitumika kwa udhalilishaji watoto na wanawake kwa kuchapisha taarifa na picha kwa lengo la kuwakashifu na kuwachafua katika jamii.

Mitandao ya kijamii ni hudumua ambayo watu nchini na kwingineko ulimwenguni, hutumia kama njia ya kuwasiliana moja kwa moja kwa kuongea.

Imekuwa ikipigiwa kelele hasa na viongozi kuwa imekuwa ikitumika ndivyo sivyo kwa kusambaza uzushi, taarifa mbaya na potofu kwa lengo la kuchafuana na kuipotosha jamii.

Pamoja na mitandao hiyo kutumika kuunganisha watu kwa nia ya kuhabarishana mambo yanayoendelea kutokea duniani, ikiwamo siasa, michezo, sanaa pia imekuwa ikilalamikiwa kwa kusambaza picha za utupu ambazo zimekuwa zimejaa udhalilishaji dhidi ya wanawake na watoto.

Twende mbele, turudi nyuma, hayo mambo kabla ya kuanzishwa kwa mitandao hiyo kama yalikuwepo yalikuwa ni nadra sana.

Ni kumi kwa mmoja, malalamiko hayo yalikuwa yakisikika ya kuwepo kwa vitendo hivyo, hiyo inatokana na kutokuwapo kwa teknolojia ya kisasa na mambo ya utandawazi yanayosababishwa na mabadiliko ya sayansi na teknolojia yanayoendelea kutokea duniani.

Zama hizo kama ni kuchafuana kulikuwa kwa njia ya mtu kuviziwa kupigwa picha kwa lengo fulani na kuzidurufu kisha kusambaza katika maeneo yaliyokusudiwa kufikisha ujumbe dhidi ya mtu aliyechafuliwa, ikwemo kwenye baadhi ya machapisho, sehemu anakoishi, ofisini na ambako anafanyia shughuli za kujiingizia kipato.

Kwa wakati huo, ilikuwa njia rahisi kudhibiti vitendo hivyo kwa mfano kama kwenye machapisho, mtu aliyelengwa katika tukio hilo, aliweza kufungua kesi ya kukashifiwa mahakamani na kudai fidia.

Hatua hiyo kwa namna moja au nyingine, ilisaidia kuogofya watu wanaojihusisha na vitendo hivyo na huenda ikawa sababu ya kufanyika kwa namna nyingine kwa kusambaza picha tu mitaani.

Lakini tangu kuanza kutumika kwa mitandao hiyo, kumekuwapo malalamiko ya watu kuchafuliwa kupitia mitandao hiyo.

Katika siku za hivi karibuni, kila kukicha kumekuwa na taarifa zikiwanukuu viongozi wa serikali, siasa na wa dini wakikemea vitendo hivyo vya udhalilishaji hasa vikiwalenga wanawake na watoto.

Malalamiko hayo yanatokana na mitandao ya kijamii kutumika kutengeneza katika ukurasa kwa njia ya maelezo na picha kuhusu makundi hayo kuhusiana na mambo yasiyofaa kwa lengo la kuichafua.

Baadhi ya mitandao ya kijamii maarufu Facebook, Instagram na Twitter, lengo la kuanzishwa kwake ilikuwa ni kusaidia kuongeza kasi ya mawasiliano ulimwenguni.

Nayo matumizi ya simu za mkononi yamekuwa na kasi ya aina yake katika kupeana ujumbe kupitia mitandao hiyo na kusambaziana picha mbalimbali, zikiwamo zisizofaa baadhi zikiwa ni za wanawake na watoto kudhalilishwa.

Naamini matukio hayo yanayochangiwa na watumiaji wenyewe wa mitandao hiyo. Mathalani, mtu anaposti picha yake, mkewe na hata mtoto tangia akiwa mdogo na kuweka 'comment' (maoni) yake, akijisifia bila kuangalia maudhuhi ya picha yenyewe kuanzia mavazi, mwonekano na mambo mengine.

Wengine unakuta wametupia picha hizo kwenye 'status zao' (hadhi) na zinapoanza kusambaa zinakwenda kwa maudhuhi tofauti.

Hivyo jamii inapaswa kuelimishwa madhara ya kutupa picha kwenye mitandao, kwani kutasaidia kuacha kukuruupuka kwa kuiga tamaduni za wenzetu.

Jamii inatakiwa kuelimisha kutumia mitandao hiyo hasa 'simu janja' kwa lengo la kupata elimu, biashara, matangazo ya biashara, siasa, ajira, afya, matibabu na utawala.

Mitandao hiyo pia imekuwa ikilalalamikiwa kupunguza ufanisi kazini ofisini kutokana na waajiriwa kupoteza muda mwingi kuchati.

HABARI KITAIFA

# Wakulima kupewa mikopo

**Na Faustine Feliciane**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB) kupitia Mfuko wa Dhamana wa Kulima Wadogo (SCGS), imeingia makubaliano na Benki ya Biashara Tanzania (TCB) kuwezesha wakulima kupata mikopo kwenye mnyororo wa thamani wa kilimo, mifugo na uvuvi.

Kupitia mkataba huo wa miaka mitano, TADB itatoa dhamana ya asilimia 70 kwa mikopo hiyo itakayowalenga wakulima wadogo wa mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi. Jijini Dar es Salaam jana baada ya kutia saini makubaliano hayo, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema mfuko huo ulianza mwaka 2018 na ni mara ya pili kwa TADB kuingia mkataba na TCB. Alisema kipindi hicho TADB iliipatia TCB Sh. bilioni saba kama dhamana. TCB ilizitumia fedha hizo kutoa mikopo ya Sh. bilioni 34.1 kwa wakulima.

Nyabundege alisema wanufaika 2,238 walifikiwa na TCB na vikundi vya ushirika 94 vilifikiwa. Kati yao, vijana 416 na wanawake 448 walinufaika.

"Hivyo mkataba mpya tunaoingia leo (jana) tumeongeza dhamana hadi Sh. bilioni 21, lengo ni kuwezesha wakulima ambao taasisi za benki zinaogopa kuwakopesha kwa kuogopa kupata hasara. Pia kupunguza umaskini na kuongeza Pato la Taifa," alisema Nyabundege.

Alibainisha kuwa mwaka 2018, serikali iliipatia TADB Sh. bilioni 57 na kufanikisha kuzalisha hadi Sh. bilioni 250.77.

Nyabundege alisema hadi Desemba mwaka jana mikopo iliyodhaminiwa na TADB kupitia mfuko wa SCGS ni Sh. bilioni 250.77 kwa wanufaika wa moja kwa moja zaidi ya 19,400 na wanufaika wasio wa moja kwa moja zaidi ya 897,900.

Alisema wanufaika hao ni kutoka mikoa 27 na wilaya 129 za Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar ambapo zaidi ya asilimia 95 ya wanufaika wote ni wakulima, wafugaji na wavuvi wadogo.

Alisema kuwa kwa mwaka huu serikali imeiongezea TADB mtaji wa Sh. bilioni 52 ili kuwezesha mfuko huo.

Meneja wa SCGS, George Nyamrunda, alisema kuwa kwa muda mrefu kumekuwa na changamoto kwa benki kuwakopesha wakulima, wengi wakihofia kupata hasara. Kutokana na hali hiyo, serikali iliamua kuanzia mfuko huo ili kusaidia wakulima. "Tunatoa dhamana hadi asilimia 50 kwa taasisi za fedha kisha na wao wanawakopesha wakulima, lengo ni kuweka kinga kwa taasisi za benki ili zisipate hasara, mkulima anaposhindwa kurejesha mkopo TADB inafidia. Na mwaka huu tumeongeza kiwango cha dhamana hadi asilimia 70," alisema Nyamrunda.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa TCB, Adam Mihayo, alisema kuwa kupitia mkutana huo, watatanua wigo wa kutoa mikopo na kufikia wakulima wengi katika sekta za kilimo, mifugo na uvuvi kwa kuwapatia mitaji itakayowawezesha kutoka katika kilimo cha kujikimu kwenda kilimo cha biashara. Alisema tangu kuanza kwa ushirikiano kati ya TCB na TADB, taasisi za fedha zilizonufaika na mfuko huo ni 16, zikijumuisha benki za biashara, benki za kijamii na taasisi ndogo za fedha zinazotoa huduma kwa wakulima.

# Kinondoni yaita wawekezaji mradi wa Soko la Bwawani

**Na Jenifer Gilla**

MANISPAA ya Kinondoni imewaita wawekezaji kuwekeza katika jengo lililokuwa linatumika kama soko katika Mtaa wa Bwawani, wilayani Kinondoni, mkoani Dar es Salaam.

Awali majengo hayo yalipangishwa kwa wafanyabishara wadogo waliokuwa wanauza nafaka, mboga na matunda, lakini walishindwa kuendelea na biashara kutokana na changamoto ya kutopata wateja, hivyo halmashauri ikakosa mapato.

Ofisa Uwekezaji Manispaa ya Kinondoni, Shadrack Mbonika, alimwambia mwandishi wa habari hizi juzi kuwa kutokana na kupata hasara hiyo, walifanya tathmini na kubaini eneo hilo si rafiki kwa biashara ya soko, hivyo kuja na mipango mingine.

Alisema wameamua kutafuta mwekezaji atakayekodi jengo hilo na kufanya biashara moja itakayokuwa rafiki kwa maeneo hayo.

Alisema kuwa tangu watoe tangazo hilo, wamepokea zabuni mbalimbali, mbili zinaonekana kuwa na mwelekeo wanaoutaka, hivyo wanaendelea kupokea na kuchambua mpaka watakapopata inayokidhi vigezo.

"Bado tunaendelea kupokea zabuni, ninawakaribisha wawekezaji walete zabuni zao. Tunataka mwekezaji mwenye biashara inayoendana na eneo hilo ili asipate hasara na sisi tupate kodi yetu bila shaka," alisema.

Ofisa huyo alikumbusha kuwa awali walilenga jengo hilo litumike kama soko ili kuwawezesha wajasiriamali wanawake na vijana kiuchumi kupitia biashara ndogo kama vile uuzaji wa nafaka, mboga na matunda.

Meneja wa Miradi wa Taasisi ya WAJIBU, Moses Kimaro, katika mazungumzo na mwandishi, alishauri manispaa itafute namna nzuri ya kufanya ili majengo hayo yasiendelee kusababisha hasara.

Alisema kama hali sokoni itaendelea kuwa kama inavyoshuhudi sasa, serikali itakuwa imefanya uwekezaji usio na tija kwa kuwa malengo ya mapato waliokuwa wamejiwekea yatakuwa hayajatimia.

Agosti 22, mwaka jana, Nipashe ilichapisha ripoti maalum kuhusu mradi huo kukosa wateja. Soko hilo lilijengwa na manispaa hiyo kupitia mradi wa uboreshaji miundombinu katika Jiji la Dar es Salaam (DMDP) kwa gharama ya Sh. bilioni 1.2.

Nipashe ilibaini kuwa halmashauri hiyo inapata hasara ya Sh. milioni 2.6 kila mwezi kwa kuwa kati ya vibanda 33 walivyopangisha kwa Sh. 100,000 kwa mwezi ni vibanda saba tu ndivyo vilivyokuwa na wafanyabiashara na kulipa kodi, vibanda (vyumba) 26 havikuwa na wapangaji.

Kati ya vizimba 154 vilivyokuwapo katika jengo hilo, vitano tu vilikuwa na wapangaji wanaoendelea na biashara na kulipa ushuru wa Sh. 500 kwa siku, hivyo kukusanya Sh. 2,500 tu badala ya Sh. 77,000.

MABADILIKO YA TABIANCHI

# Ukuta kujengwa kuzuia maji ya bahari kuvamia makazi

**Na Robert Hokororo,** DODOMA

SERIKALI imesema imeanza hatua za kujenga ukuta katika eneo la Nungwi, Zanzibar ili kuzuia maji ya bahari kuingia kwenye makazi kutokana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira), Khamis Hamza Khamis, alibainisha hayo jana wakati akijibu swali la nyongeza la Mbunge wa Nungwi, Simai Hassan Sadiki.

Mbunge huyo alitaka kujua kama eneo hilo limekidhi vigezo vya kujengwa ukuta kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Naibu Waziri Khamisi alisema serikali kupitia Ofisi ya Makamu wa Rais inatekeleza miradi ya ujenzi wa kuta katika fukwe mbalimbali za bahari Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar.

"Eneo ambalo linapaswa kujengwa ukuta limekidhi vigezo na lina kila sababu ya kufanyiwa hivyo, tumeanza kufanya utafiti na ndio maana viongozi wa SMT na SMZ wamekwishafika pale na tumeombea bajeti, hivyo serikali ina kila sababu ya kulifanyia kazi eneo hilo," alisema.

Akijibu swali la msingi la mbunge huyo, Naibu Waziri Khamis alisema serikali itaendelea kubaini maeneo yenye changamoto kubwa ya uharibifu wa mazingira na kuyaweka katika kipaumbele ili kuyatafutia rasilimali fedha kwa ajili ya kuitatua.

Alisema mabadiliko ya tabianchi yanazidi kusababisha athari katika maeneo mbalimbali nchini yakiwamo ya ukanda wa pwani.

Katika kubainisha maeneo yaliyoathirika na kuyaweka katika vipaumbele, alisema serikali inafanya tathmini ya kiwango cha uharibifu na athari zitakazojitokeza. Ndio moja ya vigezo vinavyotumika kuweka vipaumbele maeneo yaliyoathirika katika mipango ya utekelezaji

Naibu Waziri huyo alitoa rai kwa wananchi kuacha kufanya shughuli zinazoharibu mazingira na visiwa zikiwamo uvuvi usio endelevu na kilimo cha mwani kinachoharibu mazingira.


icap Global Health

MSPH Tanzania LLC, 7th Floor, Jangid Plaza, Plot No. G6, Chaburuma Road (Off-Ali Hassan Mwinyi Road)
P.O. Box 80214, Dar es Salaam, email: **icap-tz-info@columbia.edu**
Phone: +255 (0) 22 270 0719+255 (0) 22 270 0725

**INVITATION FOR TENDER FOR COMPLIANCE AUDIT SERVICES**
**PROCUREMENT REFERENCE NUMBER ICAP/TZ/05/2022-2023**

| | |
|---|---|
| **Introduction** | MSPH Tanzania LLC, known as ICAP, is a non-governmental organization operating in Tanzania since 2004, with funding mainly from the President's Emergency Plan for AIDS Relief (PEPFAR) through the U.S. Centers for Disease Control and Prevention (CDC). ICAP at Columbia University's Mailman School of Public Health is the recipient of a five-year PEPFAR-funded cooperative agreement beginning 29th September 2021 from the Centers for Disease Control and Prevention (CDC) to support comprehensive community- and facility-based HIV and VMMC services in Mwanza region. |
| | Along with this cooperative agreement ICAP received funds to conduct the second round of the Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2022-23) during this performance period. The National Bureau of Statistics (NBS) and ICAP worked in coordination with CDC and other national stakeholders to ensure a successful implementation of THIS 2022-2023. |
| **General** | Invitation for submission of proposal for yellow book audit services. |
| | ICAP now is looking for a reputable, registered, and competent audit firm to conduct an audit of Tanzania HIV Impact Survey (THIS 2022-23) activities implemented by National Bureau of Statistics (NBS) funded by CDC/PEPFAR. Detailed specification for year 2022/2023 income and expenditures for the project is contained in the tender document which will be provided to the interested bidders upon request. |
| **Bidders will be required to submit the following documentation.** | Business introduction letter, Company profile, evidence of being registered to audit US government funding by Office of Inspector General, Valid business license, Other audit certification evidence as required by law in Tanzania and internationally, Tax identification number (tin), Valid tax clearance certificate, Value added tax registration certificate (if any), Certificate of incorporation (if any), Article of association (if any), Manufacture authorization, Memorandum of association (if any), Experience justification & a recommendation letter from reputable organization. |
| **Note** | The public tender opening will be made in the presence of all bidders or their official representatives, we encourage all bidders to attend through zoom call and Zoom Call link will be sent to all who applied in advance of the meeting. Bids not received and opened in public at the public bid opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances. The tender validity period is 14 days. Selection criteria will be lowest price, technically evaluated/ acceptable based on technical specifications and other criteria described above. MSPH Tanzania reserve the rights to disqualify any offer based on failure to follow solicitation instructions. MSPH reserves the rights to waive minor proposal deficiencies that cannot be corrected prior to award determination to promote competition, MSPH will be contacting all those that have submitted quotes to confirm contact person, address and to confirm if the bid was submitted for this solicitation. The evaluation of bids will be conducted as per MSPH Tanzania LLC – ICAP Procurement Guidelines. |
| **Application procedure** | Interested and eligible vendors should email their electronic quote via email to procurement department at **TanzaniaProcurement@cumc.columbia.edu** |
| | The Internal Tender Committee (ITC), MSPH Tanzania LLC – ICAP at Columbia University, Jangid Plaza 7th Floor – Chaburuma Road, P.O Box 80214, Dar es salaam, Tanzania, all quotes must be in Tanzania Shillings. The deadline for the submission is 10:00am East Africa Time on 28th July 2023. |
| **Important to note** | **No tender fee charged for this invitation** |

# UNFPA yapewa mil. 921/- kutekeleza mradi afya ya mama na mtoto Kigoma

**Na Sabato Kasika**

SERIKALI ya Japan imetoa Sh. milioni 921 kwa ajili ya kusaidia kuendeleza mradi wa afya ya mama na mtoto kwenye kambi za wakimbizi za Nyarugusu na Nduta mkoani Kigoma.

Mradi huo wa mwaka mmoja unaoratibiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, unahusisha pia maeneo ya jirani na kambi hizo katika wilaya za Kibondo na Kasulu.

Baada ya kutia saini makubaliano ya utekelezaji mradi huo jijini Dar es Salaam juzi, Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa alisema nchi yake imejikita kusaidia sekta nyingi nchini.

"Ushirikiano wa Japan na Tanzania umejikita katika sekta nyingi; afya, kilimo, miundombinu mbalimbali, utawala bora, viwanda na nyingine. Hata fedha tulizotoa ni sehemu ya ushirikiano huo," Balozi Miswa alisema.

Balozi huyo alisema huduma za afya ni moja ya vipaumbele vya ushirikiano wa nchi hizo mbili. Programu ya afya ya mama na mtoto mkoani Kigoma ni sehemu ya ushirikiano huo.

Aliipongeza Serikali ya Tanzania kwa juhudi zake za kuboresha huduma za afya kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa afya ikiwamo kujenga zahanati na vituo vingi vya afya.

Mwakilishi Mkazi wa UNFPA Tanzania, Mark Bryan Schreiner alisema watanunua gari maalum la kuratibu shughuli za afya ya uzazi katika eneo hilo na kutoa mafunzo kwa madaktari 25 na wauguzi 25 wanaofanya kazi katika kambi hizo na maeneo ya jirani.

Schreiner alisema katika mradi huo, watumishi 15 wa afya watapata ajira kwa ajili kutoa huduma kwa wakimbizi na watu wanaoishi karibu na kambi hizo.

"Katika utekelezaji mradi huu, kutakuwa wa utoaji elimu ya afya ya uzazi kwa wakimbizi na wakazi wa maeneo yanayozunguka kambi hizo," alisema.

Schreiner alisema walengwa wakuu wa elimu hiyo ni mabinti wanaopata mimba za utotoni ili wawe na uelewa wa kutosha kuhusu madhara yatokanayo na mimba hizo. Alibainisha kuwa wanawake na wasichana 3,000 kutoka kambi za Nyarugusu na Nduta na wakazi 3,000 wanaoishi karibu na kambi hizo, pia watapewa taulo za kike ndani ya kipindi cha mwaka mmoja.

"Mradi huu pia utanufaisha zaidi ya watu 113,000 wakiwamo wanawake, wasichana, waliojifungua wakiwa na umri mdogo, wavulana waliobalehe na watu wenye ulemavu walioko nje na ndani ya kambi za wakimbizi," alisema.

Kwa mujibu wa Dk. Majaliwa Marwa, ofisa wa UNFPA, hadi Disemba 31, mwaka jana, Kambi ya Wakimbizi Nyarugusu ilikuwa na wakimbizi 136,478 huku Kambi ya Nduta ikiwa nao 64,010.

Ofisa huyo alibainisha kuwa wakimbizi wapya walioingia katika Kambi ya Nyarugusu kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo (DRC) mwaka huu ni 14,540. Kati yao, wanawake ni asilimia 56.



Balozi wa Japan nchini, Yasushi Misawa (kulia) na Mwakilishi Mkazi wa Shirika la Kimataifa la Idadi ya Watu Duniani (UNFPA) Tanzania, Mark Bryan Schreiner wakionyesha mikataba, jijini Dar es Salaam juzi, baada ya kutiliana saini makubaliano ya ushirikiano katika utekelezaji wa programu ya afya ya mama na mtoto mkoani Kigoma. Japan imetoa Sh. milioni 921 kutekeleza mradi huo. **PICHA: SABATO KASIKA**

# RC akabidhi madawati 1,500 kukabili uhaba wa samani

**Na Hamisi Nasri, Masasi**

MKUU wa Mkoa wa Mtwara, Kanali Ahmed Abbas amekabidhi madawati zaidi ya 1,500 yenye thamani ya Sh. milioni 112.5 ili kutatua changamoto ya upungufu wa samani kwenye baadhi ya shule za msingi katika Halmashauri ya Mji Masasi.

Kanali Abbas alikabidhi madawati hayo jana wilayani Masasi mbele ya Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Reuben Jichabu, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Loutery Kanoni, wakurugenzi halmashauri za wilaya na wadau mbalimbali wa elimu, makabidhiano yakifanyika kwenye viwanja vya Shule ya Sekondari ya Wasichana Masasi.

Kanali Abbas alipongeza Halmashauri ya Mji Masasi kwa kutengeneza madawati hayo 1,500 Ili kupunguza changamoto hiyo ya upungufu wa madawati katika baadhi ya shule, hasa za msingi.

Alisema serikali inaendelea kuweka mazingira rafiki ya kujifunzia na kufundishia kwa kushirikiana na wadau, akisisitiza jamii pia inapaswa kushirikiana na serikali katika kuhakikisha changamoto za miundombinu katika sekta ya elimu zinatatuliwa.

Alisema madawati hayo yaliyotengenezwa na halmashauri yatapelekwa katika shule 31 za msingi za halmashauri hiyo na shule shikizi moja kusaidia kupunguza changamoto ya upungufu wa madawati.

Aliagiza halmashauri zote za Mkoa wa Mtwara ziige mfano wa Halmashauri ya Mji Masasi kwa kutengeneza madawati na kuyagawa katika shule ambazo zina uhaba wa samani.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji Masasi, Reuben Jichabu alisema idara ya elimu ya awali na msingi ina jumla ya wanafunzi 25,328. Kati yao, wavulana 12,555 na wasichana 12,773, wote wanauhitaji wa jumla ya madawati 8,443.

Alibainisha kuwa awali kulikuwa na madawati 6,552, hivyo kulikuwa na upungufu wa madawati 1,891 na hivyo kupitia madawati hayo 1,500 yaliyotolewa yatasaidia kuondoa upungufu wa madawati.

# Mwinyi atia saini mikataba minne ya sheria hadharani

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk Hussein Ali Mwinyi kwa mara ya kwanza jana alitia saini hadharani sheria nne ikiwamo ya huduma ndogo za kifedha ya mwaka 2023.

Hafla hiyo iliyofanyika jana katika Viwanja vya Ikulu visiwani hapa, Dk. Mwinyi alisema kitendo hicho cha kutia saini sheria hadharani ni historia mpya hatua ambayo inasaidia kuongeza uwazi ili kujenga ufahamu uliyomo katika sheria hizo.

Alisema historia ya nyuma inaonesha sheria zote zilizopitishwa na vyombo vya kutunga sheria zilikuwa zikitiwa saini ndani ya ofisi na kwamba kitendo cha kutia saini hadharani kunaimarisha utawala bora, utawala wa sheria unaoendana na misingi ya uwazi, demokrasia na ushirikishwaji wa wananchi katika uendeshaji wa mambo ya nchi.

"Leo historia tunaiweka kusaini sheria nne kwa wakati mmoja hadharani na sheria hizi zitaanza kutumika kwa mujibu wa maelekezo yaliyomo," alisema Dk. Mwinyi.

Aidha, alisema sheria hizo zimepita katika hatua mbalimbali ikiwamo kufanyika utafiti wa kina na ukusanyaji wa maoni ya wadau Unguja na Pemba na hatua hiyo muhimu, ilifanyika kabla ya kuwasilishwa katika Baraza la Wawakilishi na kujadiliwa kwa mfumo wa demokrasia shirikishi.

Sheria alizotia saini ni pamoja na mpya ya Mahakama ya Kadhi ambayo imefuta Sheria namba 9 ya mwaka 2017, awali ilifuta Sheria namba 3 ya mwaka 1985 iliyoanzisha Mahakama ya Kadhi baada ya Mapinduzi ya Zanzibar ya mwaka 1964.

Alisema pia sheria zingine ni Ukaguzi wa Umma iliyofuta Sheria ya Udhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali namba 11 ya mwaka 2003 na Sheria Mpya ya Uwekezaji ambayo ni sheria bora na nzuri katika ukanda wote wa Afrika Mashariki na Kati kwa kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji nchini.

Alizipongeza taasisi zote zilizosimamia mchakato wa utayarishaji wa sheria hizo kwa kusimamia kutayarisha sheria hizo tokea hatua za utafiti na ukusanyaji wa maoni kutoka kwa wadau.

Alisema sheria hizo pia zinaimarisha uimarishaji wa miongozo ya uazishwaji wa mifumo jumuishi wa kusimamia shughuli zote za uwekezaji, kutanua wigo wa kazi za ukaguzi ili kufikia ngazi za kitaifa na kimataifa na kubaini na kuzuia mianya ya upotevu wa fedha na matumizi mabaya ya fedha za umma.

Alisema sheria pia zinawapa uwezo wa kukabiliana na vitendo vya rushwa, kuzuwia matumizi mabaya ya mifumo inayoathiri utekelezaji wa kazi na ukaguzi na kuimarisha sekta ya usimamizi na uangalizi kwa watoa huduma ndogo za fedha. "Naamini sheria hizi mpya zitatuwezesha kupambana na changamoto zote zilizokuwa vikwazo vya kutofikia malengo yetu na kuwa chachu ya maendeleo ya moja kwa moja katika sekta husika," alisema.

Alisema pamoja na kuwapo kwa sheria hizo kutaharakisha maendeleo, lakini aliwataka watekelezaji kuongeza kasi katika kufanikisha utekelezaji wa majukumu yao na kusimamia utekelezaji mzuri wa sheria hizo.

Alisema serikali imeweka mkazo mkubwa katika uchumi wa buluu ili kusukuma mbele maendeleo ya Zanzibar na juhudi kubwa zinaelekezwa kuendeleza sekta ya mafuta na gesi na kuzitaka taasisi za sheria kuaza kuchukua hatua ya mapitio ya sheria zinazokwaza kasi ya maendeleo katika maeneo hayo ya uchumi.

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, Dk. Saada Mkuya Salum, alisema lengo la sheria hiyo ya huduma ndogo za kifedha ni kutunga masharti ya utoaji wa leseni, udhibiti na usimamizi wa huduma ndogo za fedha kwa ajili ya kudumisha, utulivu, ubora na usalama wa huduma ndogo ya fedha na mambo yatokanayo na hayo.

Alisema kutungwa kwa sheria hiyo kunatokana na historia ndogo kwa Zanzibar, mwaka 1986 serikali ilianzisha sheria ya vyama vya ushirika namba 4 ya mwaka 1986 ambayo ilifanyiwa marekebisho mwaka 1998 ili kuimarisha usajili, udhibiti na uendeshaji wa shughuli wa vyama vya ushirika nchini ikiwamo vyama vya kuweka na kukopa. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Sheria, Katiba na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, akizungumzia Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Sheria ya Mahakama ya Kadhi, alisema zitaleta faida kubwa katika jamii ikiwamo uraharakishaji wa usikilizaji wa mashauri na utoaji wa maamuzi katika Mahakama ya Kadhi.

Kuhusu Sheria ya Ukaguzi wa Umma, alisema itatanua wigo wa kazi za ukaguzi, kubaini mianya ya matumizi mabaya ya fedha au rushwa na kuongeza udhibiti wa mifumo ya teknolijia katika kulinda mali za umma.



# Ndugu wasota kusafirisha maiti

**Na Allan Isack,** LONGIDO

MKUU wa Mkoa Arusha, John Mongela ameuagiza uongozi wa Wilaya ya Longido na halmashauri kujenga chumba cha kuhifadhia maiti Kituo cha Afya Kitumbeine hadi mwishoni mwa Machi mwaka huu ili kuondoa gharama kwa ndugu kusafirisha miili.

Mongela alitoa agizo hilo juzi baada ya kupokea malalamiko kutoka kwa wakazi wa Kata ya Kitumbeine kwenye mkutano wa hadhara, wakati akiwa katika ziara yake ya kukagua utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Wakazi hao walidai kuwa kituo hicho cha afya cha kisasa, hakina chumba cha kuhifadhia maiti. "Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri na Mkuu wa Wilaya ya Longido naagiza hadi kufika Machi 30 mwaka huu muwe mmejenga chumba cha kuhifadhia maiti, kuweka majokofu yasiyopungua sita na ofisi ya mtu atakayetoa huduma hapo," alisema Mongela.

Alisema Aprili mosi mwaka huu, atakwenda Kitumbeine kuzindua chumba hicho kwa kuwa ni hitaji kubwa la wakazi wa kata hiyo na jirani.

"Mkurugenzi na Mkuu wa Wilaya hii, Serikali imetoa fedha za ujenzi wa kituo cha afya, hivyo sio kila kitu lazima ifanye, suala la kujenga mochwari liko ndani ya uwezo wenu na halmashauri sasa mchakato wa ujenzi uanze mara moja," alisema.

Akizungumza kwa niaba ya wakazi hao, Joseph Sadira, alisema mtu anapofariki dunia katika eneo hilo, wanalazimika kwenda Longido mjini au Arusha mjini kuhifadhi mwili.

"Mheshimiwa Mkuu wa Mkoa kufunga safari ya kupeleka mwili Longido au Arusha mjini kuhifadhi, wananchi wanatumia gharama, tunaomba kujengewa mochwari kwenye kituo chetu," alisema Sadira.

Katika ziara hiyo, Mongela alikagua ujenzi wa choo cha shule shikizi ya Kale, bweni la wavulana la sekondari ya Kitumbeine, kituo cha afya Kitumbeine na ujenzi wa sekondari mpya ya sayansi ya wasichana



Mkuu wa Wilaya ya Mbulu Mkoani Manyara, Kheri James (kushoto) akiangalia taarifa ya mpango wa lishe ili kujenga jamii yenye afya bora, wakati wa kikao cha tathmini ya lishe, kilichofanyika kata ya Hydom juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Shirika laondoa uchakavu wa madarasa

**Na Mwandishi Wetu,** MOSHI

SHIRIKA la AKO Tanzania Community Support limekabidhi majengo ya shule ya awali na msingi ya Sungu iliyopo Kibosho Wilaya ya Moshi, mkoani Kilimanjaro baada ya kuyafanyia ukarabati na kuondokana na uchakavu.

Mkurugenzi wa shirika hilo lisilokuwa la kiserikali, Hilda Kimathi alisema jana kuwa wamekabidhi majengo hayo ya madarasa tisa baada ya kukarabati kwa gharama ya zaidi ya Shilingi milioni 140.

"Mradi huu pia ulihusisha ukarabati wa bwalo la kulia chakula, choo cha kisasa kwa wanafunzi wa kike na wa kiume na wenye mahitaji maalum na tangi la maji lenye ujazo wa lita 5,000," alisema na kuongeza kuwa: "Katika kufanikisha mradi huu, AKO kwa kushirikiana na wafadhili kutoka nchini Ujerumani, tuliguswa kukarabati madarasa haya ili kutengeneza mazingira bora ya kujifunza na kusomea."

Alisema anaushukuru uongozi wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, kwa kuwapa ushirikiano wakati wa utekelezaji wa mradi huo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Shedrack Mhagama, alisema serikali imetoa zaidi ya Sh. bilioni mbili kwa ajili ya kuboresha miundombinu ya shule zake.

Mhagama, alisema kati ya fedha hizo, Sh. bilioni 1.9 zimetumika kwa ujenzi wa shule mbili mpya za msingi.

"Fedha hizo pia zimetumika kwa ajili ya ukarabati wa madarasa 48 ya shule za msingi. Pia, serikali imetenga fedha nyingine zaidi ya shilingi milioni 600 za ujenzi wa nyumba za walimu na ukarabati wa miundombinu ya shule," alisema.

Mhagama alilishukuru shirika hilo kufanikisha ukarabati na ujenzi wa choo kipya kwa ajili ya shule ya awali na msingi ya Sungu.

"Serikali imeweka kipaumbele kuboresha miundombinu ya shule za msingi, hivyo wadau kama nyinyi ni muhimu kutokana na ukweli ya kuwa michango yenu inaunga mkono juhudi hizo," alisema.

Awali Mkuu wa Shule hiyo, Rehempta Assey aliupongeza uongozi wa AKO Community Support kwa mchango huo na kusema utakuwa chachu kuboresha elimu inayotolewa shuleni hapo.

"Mchango huu umekuja wakati mwafaka haswa ikitiliwa maanani ya kuwa shule hii iliyoanzishwa mwaka 1970 miundombinu yake mingi ilikuwa haifai tena kwa matumizi ya binadamu, sasa tuna uhakika wa usalama tuwapo madarasani na kutachangia kuongezeka kwa ufaulu," alisema.

Mmoja wa wafadhili wa mradi huo, Ingrid Miertsch, alisema na wenzake walianza kukusanya fedha miaka mitatu iliyopita nchini Ujerumani ili kufanikisha ukarabati huo.

## Wanafunzi wasoma kwenye matope

**Na Mary Mosha,** MOSHI

AFYA za wanafunzi wa Shule ya Msingi Kiwalaa ya Halmashauri ya Wilaya Moshi mkoani Kilimanjaro ziko hatarini kwa kukumbwa na ugonjwa wa kikohozi kutokana na madarasa kujaa vumbi na matope.

Wakizungumza na Nipashe baadhi ya wanafunzi hao, walisema maisha yao yako hatarini wakati wa kiangazi madarasa yao yanajaa vumbi na tope mvua zinaponyesha.

"Mazingira ya kujifunzia ni mabaya na hayaridhishi, hauoni tofauti ukiwa nje na darasani, mvua zikinyesha maji yanaingia ndani ya madarasa na kunajaa tope, jua likiwaka kunakuwa na vumbi sana," alisema mwanafunzi Hevenlight Mrema.

Mwalimu wa Taalumu wa Shule hiyo, Flaviana Temba alithibitisha miundombinu ya shule hiyo kuwa chakavu na kuathiri utendaji kazi wa walimu na wanafunzi kukithiri kwa utoro.

"Kuna wakati unakwenda darasani vumbi linatimka mwalimu unashindwa kufundisha, inakulazimu kutoka nje hadi litulie," alisema Mwalimu Temba.

"Mvua zinaponyesha kunajaa tope, mwalimu huwezi kuingia darasani kufundisha," aliongeza kusema.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Shadrack Mhagama, alisema shule zaidi ya 100 kati ya 200 ikiwemo ya Kiwalaa zilizopo katika halmashauri yao ni chakavu kutokana na kujengwa miaka mingi iliyopita.

"Tayari serikali imeanza kuziangalia hizo shule, kwa sasa tumejenga shule mbili mpya na kuchukua wanafunzi, na tuna shule nyingine tisa zimefanyiwa ukarabati kutokana na hali ya uchakavu, matundu ya vyoo, madarasa au vyote kwa pamoja," alisema.

Alisema lengo ni kuimarisha Mradi wa Kuimarisha Ufundishaji na Ujifunzaji kwa Shule za Awali na Msingi nchini (BOOST).

# Halmashauri, bodi wamaliza mgogoro wa shamba la Kibaranga

**Na Steven William,** MUHEZA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Muheza mkoani hapa na Bodi ya Mkonge nchini, wamemaliza mgogoro wa shamba la Kibaranga uliodumu kwa muda mrefu na kukwamisha maendeleo ya zao hilo na mpango wa matumizi bora ya ardhi.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Dk. Jumaa Mhina alikiambia kikao cha baraza la madiwani cha kujadili bajeti ya mwaka huu wa fedha wa 2024/25 kuwa mgogoro huo ulimalizika hivi karibuni.

Mhina alisema kukamilizika kwa mgogoro huo, kutasaidia halmashauri hiyo kupanga matumizi bora ya ardhi, kuinua kilimo cha mkonge na kukuza uchumi wa wakulima. "Siku ya leo tulikuwa na kikao cha kurejesha mahusiano baada ya kutambua mali kwenye shamba hilo zipo chini ya Hazina na shamba ni la halmashauri, sasa tutembee kifua mbele, " alisema Mhina. Alisema baada ya kumaliza mgogoro huo, halmashauri hiyo inatarajia kufufua zao la mkonge kwenye shamba la Kibaranga.

Alisema katika shamba hilo, halmashauri hiyo itapata mapato kutoka kwa wawekezaji baada ya kukamilisha upimaji.

Madiwani Mustafa Hatibu wa Kata ya Mtindiro, Gabriel Mswagala (Kwafungo) na Mwanshamba Pashua (Viti Maalum), wameiomba halmashauri hiy kuzingatia mahitaji ya a wakulima wa machungwa na wafugaji.

Mwenyekiti wa Halmshauri hiyo, Erasto Mhina amewaomba wataalamu kushirikiana na madiwani kuandika maandiko yatakayoiwezesha halmashauri hiyo kupata fedha nje ya bajeti kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. Madiwani hao, walipitisha Sh. 47, 262,554,292 kwa ajili ya matumizi kwa mwaka huu wa fedha wa 2024/25.

Kati ya hizo, Sh. 32,479,952,000, zitatumika kulipa mishahara watumishi, utekelezaji wa miradi ya maendeleo Sh. 10,310,987,149 na mengine Sh. 1, 290,905,000.





# Wanne kortini kwa mauaji ya watuhumiwa

**Na Zatifa Ramadhani,** SAUT

WATU wanne wamefikishwa katika Mahakama ya Wilaya ya Kwimba mkoani Mwanza kujibu mashtaka ya mauaji ya wakazi wawili wa Nyamohongolo kwa kuwapiga mawe na kuwachoma moto baada ya kuwatuhumu kwa kuiba kuku.

Mbele ya Hakimu Mkazi Mwandamizi wa Mahakama hiyo, John Jagadi, Mwendesha Mashtaka, Mkaguzi wa Polisi, Juma Kiparo aliwataja washtakiwa hao kuwa ni Michael Kanzaga (19),Malimi Lutema (42),Juma Bupilipili (32) na Kulwa Wangale (43), wakazi wa Kijiji cha Malemve.

Kiparo alidai kuwa Januari 11, mwaka huu, washtakiwa hao waliwaua Yusuph Mosha (33) na Gaila Lutobeka (30), dereva bodaboda kwa kuwapiga mawe na kuwachoma kwa tuhuma za wizi wa kuku.

Alidai kitendo hicho cha kujichukulia sheria mkononi ni kinyume cha Sheria ya kanuni ya adhabu sura ya 16 kifungu namba 196 na 197 iliyofanyiwa marejeo 2022.

Washtakiwa hao hawakutakiwa kujibu chochote kutokana na mahakama hiyo kutokuwa na mamlaka kisheria ya kusikiliza shauri hilo.

Hakimu Jagadi aliahirisha kesi hiyo hadi Februari 14, mwaka huu, itakapotajwa tena.

Washtakiwa hao waliruhusiwa rumande kutokana na kesi za mauaji kutokuwa na dhamana.



Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS), Mkoa wa Shinyanga, wakirekebisha barabara ya Shinyanga-Mwanza jana, ambayo imechimbwa na wananchi wa Bugweto, wakishinikiza kuwekwa matuta kutokana na kukithiri kwa ajali eneo hilo, ambapo juzi ilitokea ajali nyingine ya waendesha baiskeli kugongwa na kusababisha kifo cha Daudi Mwandu na mwezake Wambura Mtatiro kujeruhiwa. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Magulio yakosa vyoo, watu wajisaidia vichakani

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MADIWANI wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu mkoani Shinyanga, wamelalamika magulio kukosa vyoo na wakati Serikali inakusanya ushuru, hali ambayo ni hatari kutokea mlipuko wa kipindupindu.

Walibainisha hayo juzi kwenye Kikao cha Baraza la Madiwani cha robo ya pili wakati wakiwasilisha taarifa za za kata zao na changamoto zinazokabili.

Walisema magulio mengi wilayani humo hayana vyoo, hivyo kuhatarisha kutokea kwa magonjwa ya milipuko kutokana na watu kujisaidia ovyo .

Mmoja wa Madiwani hao, James Kasomi wa Bubiki, alisema kwenye kata yake kuna magulio mawili hayana vyoo na kusababisha wananchi kujisaidia vichakani.

"Licha ya halimashauri kukusanya ushuru katika magulio tumeshindwa kujenga vyoo ni hatari sana, kwa hali hii tunawezaje kudhibiti magonjwa ya mlipuko katika maeneo ya mikusanyiko ya watu kama haya,"alisema Kasomi.

Mkurugenzi wa Halmashauri hiyo, Emmanuel Johnson, alisema magulio yambayo hayana vyoo yamefungwa ili kukabiliana na kipindupindu.

Johnso, alisema halmashauri hiyo imetenga fedha ya dharura kwa ajili ya kuanza ujenzi wa vyoo kwenye magulio yasiyo na huduma hiyo ya Nyasamba, Magalata, Mhunze na Sekeididi.

Katika hatua nyingine; madiwani hao wamelalamikia ubovu wa miundombinu ya barabara na madaraja kuwa kero kwa usafirishaji watu na mazao katika kipindi hiki cha mvua.

Kaimu Meneja wa Wakala wa Barabara Mijini na Vijijini (TARURA) wilayani hapa Mhandisi Hussein Shaweji, alisema barabara hizo zitaanza kujengwa baada ya mvua kuacha kunyesha.

# Mzazi asiyepeleka mtoto shule asizae - Serukamba

**Na Thobias Mwanakatwe,** MANYONI

MKUU wa Mkoa wa Singida, Peter Serukamba amesema mtoto aliyefikisha umri wa kuanza darasa la awali na la kwanza lazima aandikishwe na kama kuna mzazi ambaye hataki mtoto wake asiende shule basi asizae.

Serukamba alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na madiwani, maofisa tarafa, wenyeviti wa vijiji, maofisa elimu kata, watendaji wa kata na vijiji wa Halmashauri ya Wilaya ya Manyoni na Itigi katika ziara yake ya kuangalia maendeleo ya uandikishaji watoto wanaojiunga na shule za awali na darasa la kwanza.

Alisema wazazi lazima watambue kuwa ni kosa la jinai kutompeleka mtoto shule kwani kufanya hivyo ni kumkosesha haki yake ya msingi ya kupata elimu kama ilivyoainishwa kwenye Katiba.

Alisema Katiba imeainisha kwamba mzazi ambaye hajamwandikisha mtoto wake kwenda shule, atasakwa na kuchukuliwa hatua za kisheria.

Serukamba, alisema kuanzia sasa maofisa elimu kata ambao ni waajiriwa wa Katibu Tawala na Mkurugenzi wa Halmashauri, wataanza kupimwa utendaji wao wa kazi kwa mambo matano ambayo ikibainika wameshindwa kuyatekeleza basi ajira zao zitasitishwa.

"Maofisa Elimu Kata Tutaanza kuwapima kwa jinsi mnavyoandikisha watoto shuleni kulingana na Sensa ya 2022, tutawapima kulingana na watoto waliofaulu, tutawapima kwa jinsi mnavyotembelea shule kuzikagua, tutawapima jinsi mnavyo 'mobilize' watoto wapate chakula shule na tutawapima mnavyosimamia utoro shuleni," alisema.

Alisema kama kuna ofisa elimu kata ambaye anadhani hawezi kufanya kazi yake kwa ufanisi, weledi na kuleta matokeo chanya kama ambavyo serikali inataka, ajiandae kwani haiwezekani kila mwaka Mkoa wa Singida upate matokeo mabaya ya mitihani ya taifa.

"Hii habari unaamka asubuhi unapewa pikipiki na Rais Samia Suluhu Hassan unazunguka nayo unaenda kwenye mashamba yako hujui kama watoto wameingia darasani au hawajaingia kwa Singida tabia hii tunakwenda kuikomesha," alisema.

Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dk. Fatuma Mganga, alisema tatizo la kufanya vibaya kielimu katika baadhi ya shule mkoani hapa linatokana na maofisa elimu kata kutojenga utamaduni wa kutembelea shule kukagua kama wanafunzi wameingia madarasani na walimu wanafundisha.

"Watoto kufeli ni fedheha, watumishi wa umma acheni kufanya kazi kwa mazoea kiongozi haongozwi bali anatakiwa kujituma maana sisi sote tuliomba kazi serikalini ili tulete matokeo chanya," alisema

Mkuu wa Wilaya ya Manyoni, Kemirembe Lwota, ameagiza viongozi wote ambao wameshindwa kufikia malengo ya uandikishaji watoto na kushindwa kutoa ripoti waandike barua za kujieleza kwanini wasichukuliwe hatua kwa uzembe huo.




Ukurasa 12

WASOMI, WADAU WAKIDAI MAGEUZI ... Mabadiliko tija bungeni yanayoengua viti maalum, kwa mbadala wa kibajeti



**Mnapambana vita vya madanguro, huku uvutaji shisha ukiwashinda!**

Ukurasa 13

BUFE
IJUMAA FEBRUARI 2, 2023
Nipashe
BIASHARA, UCHUMI NA FEDHA

# Kuzinduliwa SGR 'kunavyonukia' kutoka alichoahidi Rais Samia alipozindua 2021

## •Mkurugenzi TRC afafanua mavuno kwa hatua

**Na Pilly Kigome**

TANGU Rais Dk. Samia Suluhu Hassan aingie madarakani, akawa na ufafanuzi wa utekelezaji wa majukumu na malengo yake kitaifa.

Mojawapo ilikuwa kuendeleza yaliyoanza na mtangulizi wake, marehemu Dk. John Magufuli, au kabla ya hapo. Imo suala la kukamilisha miradi mikubwa ya kitaifa kama reli ya kisasa maarufu SGR na ule wa umeme, Bwawa la Mwalimu Nyerere.

Hapo akaendeleza kazi hiyo, ilikofika sasa, baada ya miaka na miezi kadhaa, sasa wakati wowote akitarajia kuzindua umeme huo awamu ya kwanza Bwawa la Mwalimu Nyerere lengo ni kumaliza shida hizi kitaifa. Katika reli SGR imekamilika kati ya Dar es Salaam na Morogoro na matarajio ni Julai mwaka huu, sehemu ya huduma zake huenda zikaanza.

Mnamo Julai 14 , mwaka 2021, Rais Dk Samia akiwa na miezi kadhaa katika nafasi ya sasa, akipanda kisheria kutoka Makamu wa Rais, wakati akiweka jiwe la msingi wa reli ya SGR, kutoka Isaka hadi Mwanza akafafanua umegharimu Sh. trilioni 3.06.

Rais akaahidi utaongeza ukuaji uchumi na kwa kusafirisha haraka na kwa kiwango kikubwa cha mizigo na abira, kuliko watu hivi sasa.

Ukiwa ni urefu wa kilomita 1,605, ulitarajiwa kutengeneza ajira 11,00 kwa wakazi na kupunguza muda wa safari kutoka Dar es Salaam hadi Mwanza, kutoka saa 17 za sasa, hadi saa nane pekee.




Rais Dk. Samia Suluhu Hassan, alipozindua kipande cha reli ya kisasa, SGR, kati ya Isaka na Mwanza. **PICHA: MAKTABA.**

**HATUA ILIYOFIKIWA**

Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Reli Tanzania (TRC), Masanja Kadogosa, anaanza na angalizo kwamba, licha ya awali sekta ya usafirishaji kutoa mchango mkubwa kwenye pato la taifa, asilimia 14, bado sekta hiyo imechangia kidogo sana.

Anasema ni sehemu ya mtazamo unaomfanya Rais Dk Samia kuwa na angalizo maalum katika mradi wa SGR, serikali ya awamu ya sita ikiwekeza kiasi cha shilingi trilioni 23.3 kwenye ujenzi wa reli



Sehemu ya daraja la kisasa reli SGR kuelekea Mwanza. **PICHA: PILY KIGOME.**

ya kiwango cha kimataifa.

Kadogosa anaitaja hiyo ni kati ya Dar es Salaam hadi Mwanza na awamu ya pili ikitarajiwa, vipande vya Tabora hadi Kigoma.

Anasema, kinachofanyika sasa ni kununua na kumpata mkandarasi wa ujenzi wa reli ya Uvinza hadi Musongati, unaendeleza ushirikiano na nchi ya Burundi.

Kadogosa anaendelea kufafanua kuwa, uwekezaji unaofanywa na serikali ya Rais Dk. Samia, pia umo katika Dira ya Umoja wa Afrika ya 2063, ikilenga kuunganisha miji mikubwa yote Afrika na reli ya SGR.

Ujenzi wa SGR Tanzania, unatajwa kulenga miji mikubwa Dar es Salaam na Bujumbura (Burundi), Kalemie (DRC), Kampala (Uganda) na Kigali, Rwanda, ikifungua ukanda wa Afrika Mashariki na maziwa makuu, kuwezesha na kurahisisha ufanyaji biashara kati ya nchi hizi.

Pia, anarejea kwamba SGR ni sehemu ya utekelezaji wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi, inayosimamiwa sasa na Rais Dk. Samia, huku akifafanua:

"Katika hali ya kuukuza uchumi, ujenzi wa reli ya SGR nchini kwetu tunaweza kupata fursa za kiuchumi na kijamii ambazo tunaweza kuziweka katika nyanja kuu mbili, mosi ni fursa wakati wa ujenzi wa miundombinu na pili ni wakati wa uendeshaji wa treni.

"Mradi wa SGR umechangia pato la taifa (GDP) kwa kuongeza matumizi ya malighafi za ujenzi nchini kama vile saruji, chuma, vitendea kazi, na mnyororo wa uzabuni na ugavi."

Hapo Kadogosa anatoa mfano, mnamo Desemba mwaka jana kiasi cha mifuko milioni 20.45 ya saruji yenye thamani shilingi bilioni 286.3 na nondo kilo milioni 226 zilinunuliwa kutoka Tanzania, zimetumika kwenye mradi huo,

Inaendelea Uk 12

UCHUMI

WASOMI, WADAU WAKIDAI MWELEKEO WENYE MAGEUZI …

# Mabadiliko tija bungeni yanayoengua viti maalum, kwa mbadala wa kibajeti

• Majimbo ya wilaya, jozi ya kijinsia, Bil 200/- kuokolewa

**Na Dk. Ananilea Nkya**

IDADI yao wabunge sasa ni 393, ila wanaweza kupungua hata kuokoa mabilioni ya fedha, kodi za wananchi, endapo sheria zitakazotungwa kutokana na miswada mitatu iliyofikishwa bungeni kuhusu uchaguzi, itafuta mfumo wa viti maalum.

Hapo mbadala wake wanawake na wanaume wawe wabunge kwa kupigiwa kura. Hiyo inatimia kwa

kurekebishwa miswada hiyo ya Sheria ya Uchaguzi wa Rais, Wabunge na Madiwani, 2023; Marekebisho ya Sheria ya vyama vya siasa 2023 na kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi, 2023.

Wanaharakati watetezi wa haki za wanawake na Mtandao wa Wanawake, Katiba,Uchaguzi na Uongozi wanashauri viti maalum kufutwa, kwa sababu vinaendeleza ubaguzi, wanaopitia hapo wanachukuliwa kama wabunge daraja la pili.

Kwa mfano, ni kwa wabunge wa viti maalum hawaruhusiwi kuwa wenyeviti wa kamati za kudumu za bunge, wenyeviti wa halmashauri au kushika nafasi ya waziri mkuu.

Pia, wabunge hao wanaelezwa hawapewi fedha za Mfuko wa Maendeleo jimboni, huku hawawajibiki moja kwa moja kwa wananchi, kama walivyo wabunge wa kuchaguliwa majimboni, badala yake wanawajibika vyama vilivyowateua kuwa wabunge.

"Haya yote wanayofanyiwa wabunge wa viti maalum ni ubaguzi wa jinsia ni kinyume na katiba ya nchi yetu", anaeleza Profesa Ruth Meena, mwanaharakati anayepigania kwa miaka mingi haki za wanawake akishiriki katika vyombo vya kuamua nchini.

Msomi huyo wa sayansi ya siasa, anafafanua, Sehemu ya Tatu kifungu (120 (1) cha Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977 inasema: "Binadamu wote huzaliwa huru, na wote ni sawa.

"Kifungu 13 (1-5) kinafafanua zaidi, kwa kukataza aina zote za ubaguzi, ikiwa ni pamoja na ubaguzi wa jinsia. Muhimu zaidi Wabunge wa viti maalum kutokuwajibikwa kwa wananchi ni kutumia vibaya fedha kodi za wananchi."

Mwanaharakati Gemma Akilimali, anashauri serikali izingatie bajeti ya kijinsia, ili kuhakikisha kodi ya wananchi haitumiki vibaya, badala yake zinarudishwa kwa wananchi kufanya shughuli za maendeleo.

Anasisitiza katika uhalisia uliopo kwamba, kuwapo mfumo wa uwakilishi kwa viti maalum, kunachangia kusababisha matumizi yasiyo sahihi ya fedha za wananchi, akirejea mfano shilingi milioni 16 anazolipwa mbunge kama mshahara kwa mwezi, ndani ya miaka miaka mitano (2020 -2025) kwa wanawake 113 wa viti maalum, kunaifanya serikali kupoteza zaidi ya Sh. bilioni 108.

Hapo kunatajwa kodi za wananchi, posho, pia fedha za kiinua mgongo wamalizapo miaka mitano ya utumishi. Bunge lililopo lilianza mwaka 2020 na litakamilika, 2025.

Wabunge sasa wako 393, wanaotoka majimboni kuwawajibikia wanancni 264, kati yao kinamama wako 26 (sawa na asilimia 9.8).

Idadi ya wanawake wa viti maalum ni 113. Kwa ujumla bunge la sasa lina wanawake 142, wanaounda asimilia 36 ya wabunge wote.

Kuna wabunge 10 walioteuliwa na Rais, pia Mwanasheria Mkuu wa Serikali, huhesabiwa kisheria



Profesa Ruth Meena; mwanaharakati mzoefu wa haki za kijinsia. **PICHA: MAKTABA.**

kuwa wabunge. Katika mapendekezo yao kupata uwakilishi wenye Usawa, wanaharakati watetezi wa haki wa Mtandao wa Katiba, Uchaguzi na Uongozi, wanadai jimbo moja linaweza kuwa na wabunge wawili, kama Tume ya Uchaguzi itatumia mamlaka yake kuyagawa majimbo hayo upya.

Makamu Mwenyekiti wa mtandao huo, Mary Ndaro.

katika uchambuzi binafsi, anataja uchaguzi unapaswa kuzingatia zaidi idadi ya watu na siyo ukubwa wa eneo kijiografia.

Inatajwa, endapo wilaya za kiutawala zikageuzwa majimbo ya uchaguzi, mfumo unaopendekezwa na wanaharakati utawezesha uwakilishi wa uwiano sawa kati ya wanawake na wanaume bungeni,

Pia anasema, utapunguza idadi ya wabunge nma kupunguzia gharama za bunge, kupunguza idadi ya wabunge, jambo linalowezekana kama wilaya zitakuwa majimbo ya uchaguzi.

Anataja Tanzania Bara kwa sasa kuna wilaya 128 na Zanzibaro wilaya 10, nchi kwa jumla inakuwa na wilaya 138, ambazo zikigeuzwa majimbo ya uchaguzi, inazalisha wabunge 276 wa kuchaguliwa majimboni, nusu wanawake na nusu wanaume.

Hata hivyo, idadi ya wabunge wote inaelezwa inaweza kuongezeka zaidi, kama sheria zitakazotungwa kutokana na miswada hiyo mitatu, zitaweka utaratibu wa kuwawezesha wenye mahitaji maalum kuwa na nafasi bungeni.

Hapo kuna mfano, makundi ya wenye ulemavu wa kuona, kusikia na viungo, wakitengewa viti mfano 12 bungeni kwa kuzingatia usawa wa jinsia, bunge litakuwa na wabunge wenye ulemavu sita wanawake na sita wanaume.

Inashauriwa, sheria zitakazotungwa zielekeze kila mbunge mwenyue ulemavu, apatiwe msaidizi

kulingana na jinsia yake, hivyo kutakuwapo wasaidizi 12 wa wabunge wenye walemavu, ambao hawataingia bungeni kwa sababu siyo wabunge.

Bila shaka wapo watu wanaweza kudai kwamba, watu wenye ulemavu kuwa na uwakilishi bungeni ni gharama kubwa, lakini ukweli nao wanapinga hoja hiyo.

Hapo swali linaweza kujitokeza, "je ni gharama kati ya kumnunulia waziri magari ya kifahari ya mamilioni ya fedha za kodi za wananchi" na kumpatia mlemavu wa kuona msaidizi." Anahoji Maria Challe, mwenye ulemavu wa ngozi.

Maria anasema, "mwenye ulemavu wa ngozi anaweza kuwa mbunge wa jimbo na akafanya kazi za ubunge vizuri tu, kuliko hata baadhi ya watu wasio na ulemavu wowote,"

Anaongeza: "Kwa mfano, mimi ninachohitaji muhimu sana ni 'sun screen' (miwani maalum) niweze kuongeza nguvu ya macho kuona, vinginevyo ubunge jimboni nitauweza kabisa"

Vilevile, inajionyesha hata idadi ya wabunge akiongezwa Mwanasheria Mkuu wa Serikali na wabunge 10 wa kuteuliwa na Rais, watano wanawake na watano wanaume, bado hakutakuwapo idadi kubwa ya wabunge, kama ilivyo sasa.

Wabunge wa sasa (2020-2025) wako 393, wa kuchaguliwa majimboni 264, wanawake 26 na viti maalum 113. Kwa ujumla bunge ina wanawake 142 ambao ni asilimia 36 ya wabunge wote.

Lakini, sheria tatu zitakapotungwa za uchaguzi, kutokana na miswada mitatu iliyoko bungeni, mapendekezo ya wanaharakati wanawake yakizingatiwa, inatarajiwa idadi ya wabunge itapungua.

Hapo inamaanisha bunge litakuwa na idadi sawa ya wanawake na wanaume wenye hadhi sawa, wote wenye kuwajibika kuibua uongozi bora kuharakisha maendeleo ya wananchi.

Bunge linalopendekeza ni pale wilaya zitakuwa majimbo, kukiwapo wabunge 299. Kati yao idadi 276 inagawanywa mara mbili, nusu wanawake na nusu wanaume.

Pia, kwa uwiano huo 276, idadi 20 wanatoka Tanzania Visiwani na 256 bara. Vilevile idadi ya wengine 10, nusu wanawake na nusu wanaume, ambao watapigiwa kura na makundi ya wenye ulemavu na wengine 10, kuzingatia usawa wa jinsia ni wa kuteuliwa na Rais na mmoja ni Mwanasheria Mkuu wa Serikali. Hata hivyo, ili miswada hiyo iweze kuboreshwa kukidhi matarajio ya mtandao wa Wanawake Katiba,

Uchaguzi na Uongozi, Maria anashauri: "Katiba inaweza kufanyiwa maboresho madogo madogo kwa wakati mfupi hadi hapo mchakato wa Katiba Mpya utakapoanzishwa ."

"Ili mabadiliko chanya ya kudumu yapatikane, ni lazima tupate Katiba Mpya", anasema Dk. Helen Kijo-Bisimba, anatamka. mwanamtandao wa jinsia na haki za binadamu.

**FAIDA KUPITIA BUNGE**

Inaelezwa, utaratibu wa kila jimbo kuwa na wabunge wawili mwanamke na mwanaume, una faida ya kuepuka unyanyasaji ukiwapo kingono na ubaguzi, pia taifa linaokoa fedha nyingi za maendeleo, pia heshima kwa Rais wa sasa.

Wadau wanataja gharama za kuwahudumia wabunge zitapungua kwa sababu ya kuwa na wabunge wachache, pungufu kwa 94 dhidi ya sasa wabunge 393.

Makadirio ya wadau, ni kwamba mshahara wa shilingi milioni 16 anazolipwa kila mbunge kwa mwezi inapungua, serikali itaokoa zaidi ya shilingi bilioni 18 na kwa miaka mitano, hesabu ni shilingi bilioni 90.

Pia, wanajumuisha makadirio ya posho za vikao na kiinua mgongo, serikali itaokoa zaidi ya shilingi bilioni 200 kwa miaka mitano kwa kupunguza wabunge 94.

Madala unaotolewa, shilingi bilioni 200 zinatosha kulipia bima ya watoto wote nchini katika muda wa miaka mitano; shilingi bilioni 35 kila mwaka, bima ambayo hadi sasa haigharimiwi na serikali.

Pili, wanataja Tanzania itapata heshima Afrika na duniani, ikiwa na mfumo thabiti wa kutoa idadi sawa ya wabunge wanawake na wanaume, ikigusa maeneo muhimu kama makundi ya watu wenye ulemavu na hata wanaoteuliwa na Rais.

Mafanikio ya kutekeleza wazo hilo, pia inamuachia faida Rais Dk. Samia Suluhu kama sheria hizo tatu za uchaguzi zitkazotungwa zitazingatia pendekezo tajwa la kufuta viti maalum, badala yake wanaume na wanawake watakuwa ameacha alama njema (legacy) ya kukumbukwa na vizazi vijavyo.

Ni wazi Tanzania itakuwa imebuni mfumo bora na madhubuti wa kupata wabunge wenye uwezo wa kubuni mipango bora ya kuharakisha maendeleo ya wananchi, hata huenda miaka michache ijayo, umaskini Tanzania kuwa historia.

***Ni maoni binafsi ya ya muandaaji, mtaaluma wa habari na msomi wa shahada ya uzamifu (PhD) katika masuala ya habari na maendeleo ya taifa, akiwa mstari wa mbele kwa hatua za kijinsia nchini.**

## DK. SAMIA ALIPOWAPA DARASA VIONGOZI AFRIKA UWEKEZAJI UNAVYOPITIA VIJANA

**INATOKA UK. 11**

pia kampuni zaidi ya 1,660 zinazotoa huduma mbalimbali kwenye mradi, zimeweza kuzalisha ajira zaidi ya 20,000 za moja kwa moja na ajira zaidi ya 80,000 zisizo za moja kwa moja.

Hiyo anataja ni katika sekta za kilimo na utoaji huduma, kupitia ajira za moja kwa moja takribani shilingi bilioni 259 zimelipwa kama mshahara.

**FURSA ZILIZOPATIKANA**

Kuhusu mipango mikakati inayojumuisha; zabuni zilizotolewa kwa wazawa na ziwanufaisha kiasi cha shilingi trilioni 2.05 kwa zabuni.

Fursa zingine, ni kutoa utaalamu wa teknolojia mbalimbali katika ujenzi wa SGR na usimamizi wa miradi mikubwa kwa wataalamu, wahandisi na mafundi.

Hiyo inaelezwa ni kuwezesha nchi kuwa na wataalamu wenye uwezo na weledi mkubwa, ikiwa ni somo kutoka kwenye mradi huo. Vilevile, kunatajwa kuwapo ujenzi wa miradi mikubwa na fursa za ajira kimataifa.

Inafafanuliwa, mradi SGR umewezesha kuchangia katika uboreshaji huduma za kijamii, ambazo mpaka sasa kiasi cha shilingi bilioni 17.8 zimewekezwa kwenye huduma, zikiwamo shule, maji, afya na utunzaji mazingira.

Orodha nyingine ya manufaa inatajwa ni kulinda mazingira, Kadogosa akisema uendeshaji wa treni kisasa utatumia nishati umeme na kuondoa hewa ukaa, kupunguza gharama za usafirishaji wa bidhaa kwa asilimia 40, vilevile kuokoa matumizi ya fedha za kigeni za kuagiza mafuta nje ya nchi. Inafafanuliwa kwamba, mradi wa SGR utapunguza hewa ya ukaa kwa asilimia kati ya 30 na 40. Kwa mujibu wa Kadogosa, hadi kufika miezi miwili iliyopita, Novemba 2023, ujenzi wa mradi wa SGR ulikamilika kwa wastani ufuatao, asilimia zake kwenye mabano:

Kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (98.2%);, Morogoro - Makutupora ( 96%); Makutupora - Tabora (13.19%), Tabora - Isaka (5.3%), Isaka - Mwanza (47.4).

Wakati lengo lililopo ni huduma hiyo ya safari kuanza Julai mwaka huu, Kadogosa anasema Wizara ya Uchukuzi inaendelea kusimamia kwa karibu mradi, huku dhamira ya Rais Dk. Samia ni kuendeleza uchumi na demokrasia kwa nchi za Afrika Mashariki, COMESA na SADC, ukihusisha moja kwa moja na reli ya SGR. Hadi sasa, Tanzania imekuwa kivutio cha miradi hata nchi kama za Rwanda, Burundi, DRC, Zambia, Uganda na Ethiopia kutuma wataalamu wake kujifunza.

TAFAKURI YA MLALAHOI

## Mnapambana vita vya madanguro, huku uvutaji shisha ukiwashinda!





KUNA wakati mtu unaweza kujiuliuza mambo mengi lakini usipate majibu ya haraka na kuacha yaendelee tu kama yalivyo, kutokana na muktadha ulivyo.

Mambo mengine huwa ni ya kushitua na mengine ya kushangaza, lakini ndivyo maisha yanavyokuwa, kwani yana mchanganyiko wa matukio, dhana na fikra za wamiliki wake.

Hebu fikiria ghafla unasikia kuna mkuu wa mkoa au wa wilaya fulani kachukuana na kamati yake ya usalama, kwenda mtaani kuvunja madanguro au kukamata makahaba.

Na wanakwenda huko na mabunduki na pingu kukamata watoto wa kike kwa tuhuma kuwa wanajiuza na kuwataka wajiajiri, ambao umekuwa ni wimbo wanasiasa.

Utawasikia majukwaani wakiwahimiza vijana kujiajiri na kuacha kuzurura na kujiuza huku wakijua fika, kuwa kujiajiri kunahitaji mtaji na kama wao wasingekuwa na nafasi za kisiasa wasingekuwa na ajira.

Wanavunja madanguro na kukamata watoto wa kike na kisha kuwaacha hawana pa kukaa, hawana chakula na hawana makazi, kwani kilichokuwa kikiwaingizia kipato ndicho kimeondoka.

Sidhani nitafikiriwa kuwa naunga mkono madanguro na ukahaba, la hasha, naunga mkono mtu kujipatia kipato cha kuendesha maisha yake lakini kiwe halali.

Nasita kusema kuwa ukahaba au madanguro ni halali, lakini pia kisheria sidhani kama ni haramu na ndiyo sababu sijapata kusikia fulani kafikishwa mahakamani kwa kujiuza bali kwa uzururaji.

Unakuta eti polisi na bunduki yake anavamia baa kusaka wasichana wanaojiuza; huku na kule anasababisha usumbufu kwa jambo ambalo halina maana kabisa na kiongozi akiulizwa, anasema sikuagiza hayo.

Na kweli hakuagiza, lakini kama mkubwa anatarajia nini anaposema kazi hiyo hairuhusiwi na ipigwe vita, huku akijua askari wetu ni wa aina gani, baadhi yao wakitumia fursa hiyo kutisha na kujipatia kipato haramu.



**NA JOSEPH KULANGWA**
Simu: +255 713 410008
barua pepe: kulangwasos@gmail.com

Yupi sasa ni halali hapo, anayejiuza na kujipatia kipato, au anayetisha kwa bunduki na kujipatia kipato? Nani mkorofi hapo, mwenye mwili wake au mwenye bunduki?

Badala ya kukimbizana mitaani kama alivyopata kusema Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere, viongozi wawatafutie shughuli za kufanya, watafanya ili mradi wanapata kipato chao cha kila siku.

Najiuliza wakati mwingine, hivi serikali ingewataka wakazi wa Ngorongoro kuhama kwa hiari bila kuwapa eneo lingine la kukaa Msomera, wangehama kweli? Bila shaka wasingehama.

Kama ndivyo, kwanini makahaba wafukuzwe au wakamatwe na madanguro yavunjwe usiwepo mbadala, ili waendelee na maisha yao bila kufanya yanayoichefua serikali?

Cha kuchekesha, nguvu kubwa inatumika huko, huku upande mwingine ukiendelea kuoza! Hivi sasa tunapiga vita matumizi ya dawa za kulevya miongoini mwa vijana, lakini tunaachia matumizi ya shisha!

Nakumbuka vizuri sana Julai, 2016 kwenye futari ya madhahebu ya Shia iliyofanyika Dar es Salaam, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa alipiga marufuku uvutaji shisha, akiliagiza Jeshi la Polisi kuhakikisha ulevi huo unapotea kabisa nchi nzima.

Katika kuelimisha umma kuhusu ubaya na madhara ya shisha, Waziri Mkuu akasema kilevi hicho huchanganywa na pombe zingine vikiwamo viroba, ambavyo alhamdulilahi vilipigwa marufuku vikatoweka.

Majaliwa alifanya hivyo siku moja tu baada ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Paul Makonda naye kupiga marufuku shisha na uvutaji sigara hadharani.

Hivi shisha imetoweka? Haipo? Hebu nendeni kwenye baa mjionee kinachoendelea kuhusu shisha. Inavutwa sawa kabisa na sigara zingine na sawa na vinywaji vingine halali vikali, vichungu na vitamu.

Hayo yanafanyika, sijawahi kusikia marufuku ile ya mwaka 2016 imetenguliwa kokote na aliyekataza bado hajahalalisha shisha ambayo sasa inachanganywa si tu na bangi, bali na mihadarati mingine.

Daktari mmoja nimemsikia akisema tumbaku inayowekwa kwenye mtungi mmoja wa shisha, ni sawa na sigara 200! Hebu fikiria vijana wanaotumia shisha wanajiweka wapi? Taifa linajielekeza wapi?

Kwanini badala ya polisi kuingia baa kusaka wasichana wanaojiuza, lisiende huko kukamata shisha na kuvunjavunja mitungi hiyo, ili kuokoa vijana wetu wasitumbukie kwenye uraibu wa mihadarati na kuharibikiwa? Eh Mungu tusaidie hii kazi ya shisha isiendelee!

UCHUMI

# Kata kinara wa ukatili kijinsia Dar, ikianika kuna mzizi wa kiuchumi

## •Kilio kikuu watoto, wenyeji rasmi kupambana



Wanafunzi wa elimu ya msingi, katika mahafali katika shule iliyoko katika Kata ya Msongola. **PICHA: MAKTABA**

**Na Mwandishi Wetu**

INAPOTAJWA ukatili wa kijinsia, inaangukia katika mambo yanayoweza kupunguza kasi ya ukuaji uchumi kwa mtu mmoja mmoja, kikundi cha watu, familia au serikali kwa ujumla.

Mtu aliyefanyiwa ukatili huo anaweza kuathirika kiakili na kimwili, pia inategemea na aina ya ukatili uliofanyika na pale inapoachwa kukua, huathiri ukuaji wa kiuchumi kwa familia husika, unaifanya kuwa dhana ya kupigwa vita kwa nguvu zote kitaifa.

Tendo hilo linatajwa kuangukia jinsia zote, mwanamke au mwanaume, lengo ni kumdhuru au kumkera kisaikolojia kimwili,kiafya, kingono na kiuchumi, kwa yule anayetendewa.

Utafiti mwingi unaonyesha kuwa wanawake na Watoto, ndiyo waathirika wakuu wa masuala ya ukatili wa kijinsia. Hapo ndipo katika Kata ya Msongola, jijini Dar es Salaam, nayo inaguswa na changamoto hiyo mahsusi kinamama na watoto.

Ofisa Ustawi wa Jamii Kata ya Msongola, Joliga Msekwa, anasema kata hiyo imeguswa na ukatili wa aina zote, ukiwamo wa kingono, kimwili na kisaikolojia.

Kimwili, ofisa huyo anasema Msongola wanakabiliwa na changamoto ya ukatili, ambao wanawake wameendelea kuketwa, jambo ambalo liko katika marufuku kitaifa na kufanywa kampeni ya kuizuia.

Vilevile anataja kingono, Msekwa anasema huko Msongola hilo linafanyika hadi kwa watoto wadogo wenye umri wa miaka mitatu mpaka saba.

Akisimulia huku akitokwa na machozi, mkasa wa mtoto wa miaka saba kubakwa na wanaume wanne, Msekwa anasema mtoto huyo alianza

kutendewa ukatili huo akiwa na umri wa miaka mitatu, hata akazoea tendo la wanaume hao kila mara mpaka sasa ana miaka saba.

"Mtoto huyo ambaye jina linahifadhiwa, alikuwa akiishi na bibi yake ambaye maisha yao ni ya tabu kidogo. Hivyo, bibi hulazimika kwenda kutafuta riziki na kumuacha nyumbani, hivyo mtoto anaamua kwenda kucheza nyumba jirani kuangalia televisheni," anasimulia Msekwa.

"Wanaume humchukua mtoto huyo na kumpakata miguuni na kuanza kumfanyia vitendo vya ngono kwa kuwa hakukuwa na mtu wa kumfuatilia.

> "Hivyo, kuna wakati alilazimika kuomba hela ili akawape wanaume wamfanyie kitendo hicho, ndipo alipofika umri wa miaka saba,alikutana na unyama wa kubakwa na wanaume wanne...inaumiza sana!" anasema.

"Alipata maumivu lakini mwisho wa siku alizoea na akawa hawezi kukosa tendo hilo hivyo aliwafuata ili wamfanyie kitendo hicho. Mtoto aliendelea kukua akiwa mtaalamu wa mambo hayo.

"Hivyo, kuna wakati alilazimika kuomba hela ili akawape wanaume wamfanyie kitendo hicho, ndipo alipofika umri wa miaka saba,alikutana na unyama wa kubakwa na wanaume wanne... inaumiza sana!" anasema.

Msekwa anasimulia, mtoto huyo alipotea nyumbani kwa siku nzima bibi yake alimtafuta mwisho aliamua kufika katika Ofisi ya Ofisa Ustawi wa

Jamii Kata ya Msongola, kutoa taarifa na kuomba msaada.

Anasimulia siku iliyofuata mtoto alirudi akiwa anaumwa sana, lakini bibi huyo alipomuuliza mtoto hakujibu kitu, hali iliyomfanya bibi yake ahisi ni kiburi binafsi na kuanza kumchapa.

Msekwa anasema, lakini alipofikishwa kwa Ofisa Ustawi akaeleza vyote, ndipo walipochukua hatua za kisheria na watuhumiwa kufikishwa katika

vyombo vya sheria.

Anasema, ni kesi nyingi zikiwamo za wazazi kuwachoma moto watoto katika sehemu za mikono, masikio na mdomo huwafikia, huku kwa

upande huo ,baadaye hakutaka kuandikwa jina gazetini, akinena kwa uchungu, sasa anawasihi wanaume kuacha tabia za kufanya ukatili kama huo.

"Naiomba serikali itoe elimu kwa jamii kuhusu masuala ya ukatili watu wajue ukatili ni nini, aina za ukatili na madhara yake jamii ikiwa na uelewa inaweza kuachana na vitendo hivyo," anatamka.

**JUKWAA LA UWEZESHAJI**

Mwenyekiti wa Jukwaa la Uwezeshaji Wanawake Kiuchumi Kata ya Msongola, Salome Mwasamale, anasema wamejipanga mwaka huu, kuhakikisha wanakomesha ukatili huo wa kijinsia, hata kuifanya Msongola salama, jambo wanaloamini linawezekana.

Salome anatamka hayo kwenye uzinduzi wa jukwaa hilo, akizundua kampeni maalum ya kupinga ukatili katika kata ya Msongola yenye kaulimbiu "pinga ukatili wa kijinsia,wanawake wawezeshwe kiuchumi".

Anasema, jukwaa lao limeandaa mikakati kwa kushirikiana na viongozi wa serikali za mitaa, kuhakikisha inatokomeza tatizo hilo Msongola.

Anataja baadhi ya mikakati yao, ni pamoja na kutoa elimu ya kujijengea uwezo jamii kuelewa vizuri aina za ukatili wa kijinsia, madhara na viashiria, akiamini hilo linaweza kufanikisha miradi mingine kirahisi.

"Jukwaa kata ya Msongola kwa kushirikiana na serikali, tumejipanga vizuri kuhakikisha tunatokomeza kabisa ukatili wa kijinsia katika kata Yetu.

"Hatufurahii kusikia vitendo vya kikatili vinavyoendelea vya watoto wadogo kubakwa au kuchomwa na vitu vyenye ncha kali mwilini, hili ni lazima tuhakikishe tunaliondoa kabisa," anasema.

Akizindua kampeni hiyo ya kupinga ukatili wa kijinsia Kata ya Msongola, Mkurugenzi wa taasisi ya kijamii ya Himiza, Prisca Ngwashemi, anasema katika Serikali ya Awamu ya Sita, chini ya Rais Dk. Samia Hassan Suluhu, imejipanga vizuri kuhakikisha inatokomeza ukatili wa kijinsia.

Hivyo anatamka kuungana na viongozi wa jukwaa kuhakikisha kampeni hiyo inafanikiwa kwa asilimia 100, akinena kuwa hadi sasa serikali imeboresha mbinu za utendaji kazi hivyo wananchi wasiogope kutoa ushirikiano kwa kuwa, hakuna atakayedhurika kwa kutoa taarifa, kwa kuwa inabaki kuwa siri kubwa.

Hadi sasa, Mkoa wa Dar es Salaam unatajwa kuwa na ongezeko kubwa la matukio ya ukatili huku Kata ya Msongola, ikitajwa kuwa kati ya kata tatu zinazoongoza kwa ukatili wa kijinsia ikiwemo Kitunda, Kivule na Msongola.





# Mradi kuwawezesha walemavu kielimu

**Na Valentine Oforo,**
DODOMA

CHUO cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP) kimeanza kutekeleza mradi maalumu wa kujenga mazingira wezeshi ya kujifunzia wanafunzi wenye mahitaji maalum ili kuwezesha kupata elimu bora.

Mpango huo unaolenga kutoa elimu jumuishi unatekelezwa chini ya ufadhili wa Mradi wa Elimu ya Juu kwa Mageuzi ya Kiuchumi (HEET) na vyanzo vya ndani vya taasisi hiyo.

Mkuu wa IRDP, Profesa Hozen Mayaya alisema kuwa taasisi hiyo inayofanya kazi chini ya Wizara ya Fedha, imeamua kutekeleza mradi huo ili kuhakikisha wanafunzi wenye mahitaji maalum wanapata haki zao za kisheria za elimu bora.

Prof. Mayaya, alisema taasisi ipo katika mchakato wa kuajiri walimu wenye weledi wa kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalumu.

"Katika waraka wetu unaohusu utaratibu wa utumishi wa chuo, tumeomba kuajiri wataalamu mahiri kwa ajili ya kuwafundisha wanafunzi wenye mahitaji maalum, na tayari tumepeleka waraka huo kwenye Ofisi ya Rais, Manejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ajili ya kuidhinishwa," alisema Mayaya. Alisema taasisi hiyo inafanya kazi ya kuwatambua wanafunzi wenye ulemavu ili kuwasaidia kulingana na changamoto za kimwili walizonazo.

"Lengo ni kuhakikisha chuo kinakuwa sehemu bora na rafiki kwa wakazi na kutoa elimu bora kwa wanafunzi wote walioandikishwa, bila kujali hali zao za kimwili," alisema.

Dk. Sagumo Malenda, Mratibu wa Elimu Jumuishi (EI) chini ya Mradi wa HEET katika taasisi hiyo, alisema kwa sasa chuo kina zaidi ya wanafunzi 27 wenye mahitaji maalumu.

Alisema idadi hiyo inajumuisha wale wenye ulemavu wa kusikia, viungo, uoni hafifu na wa ngozi (albino).

"Katika awamu ya kwanza, IRDP ilipokea takribani shilingi milioni saba kutoka mradi wa HEET kwa ajili ya kuhudumia wanafunzi wenye mahitaji maalum, " alisema

Alisema pamoja na huduma nyingine, mradi huo unajikita kuwapatia wanafunzi hao vifaa vya kuwasaidia na chuo kujenga miundombinu rafiki.



Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson (kulia), akiagana na wageni wake baada ya kumalizika hafla ya kumpongeza kwa kuchaguliwa kuwa Rais wa Umoja wa Mabunge Duniani, iliyofanyika katika Ukumbi wa Pius Msekwa, jijini Dodoma jana. Kushoto ni Katibu Mkuu wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT), Mwalimu Japhet Maganga. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wazazi watakiwa kupinga ndoa za utotoni

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

JUMUIYA ya Wazazi ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) Mkoa wa Singida imewataka wazazi kupinga ndoa za utotoni na kuagiza wanaojihusisha na vitendo hivyo wachukuliwe hatua.

Mwenyekiti wa Jumuiya hiyo mkoani hapa, Bertha Nakomolwa alitoa kauli hiyo jana wakati akizungumza na wakazi wa Kata ya Ughandi Halmashauri ya Wilaya ya Singida, ikiwa ni sehemu ya Maadhimisho ya Miaka 47 ya kuzaliwa kwa CCM.

Nakomolwa, alisema kumuozesha mtoto wa kike ni ukatili dhidi yake kwa kuwa anatakiwa kusoma na sio kuwa mama wa familia katika umri mdogo.

Mwenyekiti huyo aliwataka madiwani na watendaji wa kata mkoani hapa kuwasomea taarifa za mapato na matumzi wananchi na kutatua changamoto zinazowakabili.

Alisema ni lazima wananchi wasomewe mapato na matumzi ili kuondoa sintofahamu katika kipindi cha kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa na uchaguzi mkuu mwakani.

Alisema Serikali inatekeleza miradi mingi kwa kutumia fedha nyingi, hivyo ni muhimu taarifa za mapato na matumzi ziwe wazi kwa wananchi ili wafahamu.

Nakomolwa aliwataka wanawake kujitokeza kwa wingi kuchukua fomu za kugombea uongozi katika uchaguzi wa serikali za mitaa utakaofanyika mwaka huu.

Wakati wa maadhimisho hayo, wanachama wa jumuiya hiyo na wananchi walipanda miti kwa ajili ya kutunza mazingira.

# Taarifa kisheria kupatikana popote bila kutumia mtandao

**Na Renatha Msungu,**
DODOMA

MTENDAJI Mkuu wa Mahakama, Profesa Elisante Ole Gabriel amezindua mfumo wa sheria mfukoni kwa ajili ya kumwezesha mtumiaji kupata taarifa za kisheria popote bila kutumia mtandao.

Akizungumza juzi wakati wa uzinduzi wa mfumo huo uliofanyika kwenye Maonyesho ya Wiki ya Sheria, alisema mfumo huo utawezesha mtu kuwa na sheria kiganjani bila kutumia mtandao.

"Mfumo huo unaweza kutumika katika simu, kishikwambi na laptop bila kuwa katika mfumo wa internet , inakuruhusu zile nyaraka zote kama hukumu, sheria na nyaraka nyingine nyingi kuzifanyia kazi na unapofika sehemu zenye mtandao unaunganisha, zinajipakua zinakamilisha zile kazi ambazo zingetumia muda mwingi kusubiri mtandao ," alisema

Alisema huo ni mwendelezo wa mageuzi makubwa ya kitehama yanayotokea katika nchi.

Alisema serikali imesaidia kupata rasilimali fedha na rasilimali watu. Alisema kuwa Jaji Mkuu wa Tanzania, Profesa Ibrahim Juma amekuwa na mchango mkubwa kwa kuweka msukumo na kuondoa mlolongo kwa wananchi kupata haki mahakamani.

"Haya ni mageuzi makubwa sana, wito wangu kwa mahakama kuchangamkia fursa zinazotokea, kwani mfumo huo unaifanya mahakama kuwa tofauti na mahakama nyingine," alisema .

Alisema mfumo wa TanzaLII duniani unatembelewa kwa asilimia 82.4 ikilinganishwa na mifumo mingine .

"Utaona ni jinsi gani mfumo wetu umewaacha mbali wengine," alisema.

Mkurugenzi wa African LII na mwanzilishi mwenza wa sheria Afrika, Mariya Badeva, alisema kuwa ushirikiano uliopo una lengo la kuendeleza ufikiaji wa taarifa za kisheria barani Afrika na kusambaza taarifa za kisheria kwa uendelevu.

Alisema kuwa sheria ya mfukoni inawakilisha ubunifu uliondaliwa kutoa suluhisho la vitendo na kujibu mahitaji mahususi ya mataifa ya Afrika na Tanzania.



# Vijana 380 wahitimu mafunzo ya uanagenzi MUST

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

VIJANA 380 waliokuwa wakisoma mafunzo ya uanagenzi awamu ya tatu katika Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) wamehitimu mafunzo hayo.

Mafunzo hayo yalikuwa yanafadhiliwa na Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu. Vijana hao wamehitimu mafunzo hayo katika fani 14 tofauti za ufundi ambazo zimewawezesha kupata ujuzi utakaowasaidia kujiajiri wenyewe na kuajiriwa kwenye taasisi mbalimbali.

Akizungumza na wahitimu hao wakati wa mahafali, Kaimu Mkurugenzi wa Jiji la Mbeya, Elia Fwalo aliwataka wahitimu hao kwenda kufanya kazi kwa bidii na kwa uadilifu ili waaminiwe na waajiri wao pamoja na jamii watakayokuwa wanaihudumia.

Aidha aliwataka kujiunga katika vikundi ili waweze kukopesheka na kupewa tenda ya kutekeleza miradi mbalimbali ya serikali ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya elimu, afya, maji na barabara ambayo inahitaji ujuzi wao.

Alisema katika utekelezaji wa miradi ya serikali kwa mfumo wa kutumia mafundi wa mitaani huwa inatokea tatizo la utekelezaji wa miradi hiyo kwa kujengwa chini ya kiwango kutokana na mafundi wanaowatumika kutokuwa na mafunzo.

"Hawa mafundi wasio na ujuzi mara nyingi wanafanya kazi zisizo na ubora, ukifika pale ofisini kwa mkurugenzi tumeweka orodha ya mafundi, waliofanya kazi vizuri na vibaya, kwa hiyo sitegemei nyie kuingia kwenye orodha ya mafundi wanaofanya vibaya na badala yake mkafanye vizuri," alisema Fwalo.

Makamu Mkuu wa Chuo cha MUST Taaluma, Prof. Godliving Mtui alisema katika awamu ya tatu ya mafunzo ya uanagenzi chuo hicho kimetoa mafunzo kwa vijana 1289.

Alisema mafunzo hayo hutolewa kwa muda wa miezi nane ikiwa ni pamoja na miezi sita ya nadharia pamoja na miezi miwili ya mafunzo kwa vitendo.

Alisema Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano unajielekeza kujenga uchumi shindani na uchumi wa viwanda kwa maendeleo ya watu hivyo mafunzo hayo yamekuja kwa wakati muafaka utakaokamilisha lengo hilo.

Katika risala ya wahitimu hao iliyosomwa na Doreen Kileo aliiomba serikali kuwapatia mikopo nafuu ambayo itatumika kama mitaji ya kununulia vifaa ili kujiendeleza kiuchumi watakapokuwa wanatekeleza miradi.

Vilevile aliomba serikali kuwapa kipaumbele cha kazi kwenye miradi inayotekelezwa katika maeneo mbalimbali ili kuwawezesha kiuchumi na kutoa mchango wao katika taifa kama vijana waliosomeshwa bure na serikali.

Baadhi ya fani ambazo vijana hao wamehitimu ni pamoja na TEHAMA, ufundi magari, ufundi umeme, ufundi bomba, useremala, ubunifu wa mitindo na ushonaji nguo, uchomeleaji, ufundi washi, pamoja na huduma za hoteli na utalii.



Mjasiriamali mnufaika wa Mpango wa Taifa wa Kunusuru Kaya Masikini (TASAF), katika kijiji cha Nzunda, Kata ya Ndato, wilayani Rungwe mkoani Mbeya akiendelea na biashara yake katika soko la kijiji hicho juzi, ambapo mtaji wa kuendeshea shughuli hiyo ni sehemu ya ruzuku aliyopewa kupitia mpango huo. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# Uhamisho walimu vijijini wawakera madiwani Mbeya

**Na Nebart Msokwa,** MBEYA

MADIWANI katika Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya wamelalamikia uhamisho wa walimu kutoka vijijini kwenda mjini wakisema hatua hiyo inasababisha uhaba wa watumishi hao vijijini pamoja na kiwango cha ufaulu kuporomoka.

Hivyo, wameiomba serikali kupitia Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI) kutatua kero hiyo kwa kujaza nafasi zinazoachwa baada ya walimu hao kuhamishiwa mjini ili kuondokana na tatizo hilo

Walitoa malalamiko hayo mwishoni mwa wiki kwenye kikao cha robo ya pili cha baraza la madiwani wa halamashauri hiyo kilicholenga kujadili mipango ya kamati mbalimbali ikiwemo masuala ya elimu, afya na maji.

Diwani wa Kata ya Izyira, Abel Mwazembe alisema pamoja na jitihada za serikali kupeleka walimu vijijini lakini wengi wao wanahamia mjini kwa sababu mfumo unaruhusu mtu yeyote kushughulikia uhamisho huo yeye mwenyewe.

Aliiomba Serikali kuzingatia uwiano wa kijinsia wakati walimu wanapopelekwa kwenye shule ili kuwahudumia hasa wanafunzi wa kike huku akieleza kuwa Shule ya Sekondari ya Izyira ilikuwa na mwalimu mmoja pekee wa kike ambaye naye amehama.

Diwani wa Kata ya Utengule Usongwe, Yona Ntunjilwa aliishauri Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Mbeya kuwasiliana na Ofisi ya Rais TAMISEMI ili kupata ufumbuzi wa tatizo hilo.

Alisema kata yake ya mjini imekuwa ikipokea idadi kubwa ya watumishi wa umma kutoka vijijini wenye hati ya matibabu za matatizo ya kiafya ili kusaidia uhamisho wao.

"Uhamisho wa mfumo umekuwa tatizo kubwa, shule za vijijini zilizoathirika zimesalia bila uwiano sawa kati ya walimu na wanafunzi, unakuta shule yenye wanafunzi 350 lakini walimu watatu, hatuwezi kuwa na maendeleo ya kielimu kwa njia yeyote ikiwa hali hii itaendelea," alisisitiza Ntunjilwa.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Ezekia Shitindi aliwaagiza maofisa elimu kulifanyia kazi suala hilo, ikiwa ni pamoja na kushauriana na Ofisi ya Rais-TAMISEMI kabla ya uhamisho huo kufanyika.

Mwakilishi wa Katibu Tawala Mkoa wa Mbeya, Eliah Chigoji alisema ujio wa mfumo haujabadilisha taratibu za watumishi hivyo basi kila mmoja anapaswa kuzingatia maelekezo yaliyopo na kuahidi mkoa kushughulikia changamoto zilizojitokeza.

# Sekondari Manyunyu wajengewa choo, chumba cha kujisitiri

**Na Mwandishi Wetu,**

NJOMBE

TAASISI ya Flaviana Matata imekabidhi choo chenye matundu 12 na chumba maalum kwa ajili ya wasichana kujisitiri pamoja na sehemu ya kuchomea taka zikiwemo taulo za kike katika Shule ya Sekondari Manyunyu iliyopo mkoani Njombe.

Pia imekabidhi sehemu ya kunawia mikono, chumba kwa ajili ya wanafunzi wenye mahitaji maalum shuleni hapo kwa ufadhili wa Segal Family Foundation.

Akizungumza na waandishi wa habari kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Prof. Adolf Mkenda, Mkurugenzi wa Elimu Maalum Tanzania, Dk. Magreth Matonya, alipongeza kazi iliyofanywa na taasisi hiyo katika mikoa tofauti nchini.

Alisema taasisi hiyo imeendelea kuwa mstari wa mbele katika kutatua kero mbalimbali zinazowakabili watoto wa kike kufikia ndoto zao.

Pia alisema taasisi hiyo imekuwa ikisaidia kuhamasisha wanajamii na serikali kuboresha upatikanaji wa elimu bora kwa watoto wa kike kwa kuboresha mazingira ya shule.

Alisema kuwa pia taasisi hiyo imekuwa ikifadhili masomo kwa watoto wa kike wanaotoka katika mazingira magumu, kutoa elimu ya hedhi salama na afya ya uzazi, ugawaji wa taulo za kike mashuleni, utoaji wa vifaa vya kujifunzia na kufundishia, vilevile kuwawezesha mabinti waliokatisha masomo kwa sababu mbalimbali kurejea mashuleni chini ya sera ya 'Re-Entry',.

Katikati ya hafla hiyo, Waziri Prof. Mkenda alipiga simu na kuongea na hadhira iliyohudhulia tukio hilo na kusema kuwa: "Nimefurahi sana kuendelea kushuhudia kazi nzuri inayoendelea kufanywa na taasisi hii chini ya mkurugenzi wao Flaviana na tunaendelea kuona matokeo chanya yanayoendelea katika maisha ya wanafunzi hususani mabinti," alisema Prof. Mkenda na kuongeza kuwa;

"Upatikanaji wa huduma bora za usafi wa mazingira ni haki ya msingi kwa kila mtu na ni jukumu letu sote kuhakikisha kuwa wanafunzi wana rasilimali wanazohitaji ili kufaulu kielimu na kuishi maisha yenye afya," alisema Prof. Mkenda.

Naye Mkurugenzi wa Taasisi ya Flaviana Matata, Flaviana Matata alisema taasisi hiyo inafanyakazi katika mikoa mitano ukiwamoNjombe katika kusaidia serikali husasani kuwajengea uwezo watoto wa kike katika kutoa elimu ya hedhi salama.

"Mpango huu sio tu unaunda mazingira bora na safi lakini pia unaondoa vikwazo vinavyowazuia kuendelea na elimu yao. Tunaamini kwa kuendelea kutatua changamoto hizi kutachochea mabadiliko chanya sasa na kwa miaka ijayo." alisema



# Wanaobandika kope hatari kwa ugonjwa wa macho

**Na Mwandishi Wetu**

WANAWAKE wametakiwa kuacha tabia ya kubandika kope za bandia kwenye macho kwa sababu zinashabihiana na ugonjwa wa macho mekundu unaoendelea kutikisa nchini.

Wito huo ulitolewa juzi na Mratibu wa Huduma za Msingi za Matibabu ya Macho, Rajab Mohammed Hila wakati akizungumzia kuhusiana na kusambaa kwa ugonjwa huo visiwani Zanzibar unaosababishwa na virusi aina ya Adenovirus.

Dk. Hila, alisema kope hizo za bandia ni kati ya vitu vinavyoweza kuchangia kwa maambukizi ya ugonjwa huo.

Hata hivyo, hakufafanua zaidi ya kutoa tahadhari kwa wanawake, hususani wasichana wanaotumia kope hizo kwa ajili ya kuongeza urembo.

Akizungumzia kuhusu athari za muda mrefu za ugonjwa huo iwapo hautapatiwa tiba mapema, alisema ni kupoteza uoni wa macho kwa sababu virusi vina uwezo wa kushambulia kioo cha jicho.

Alisema wagonjwa wengi wa macho hawafiki hospitali kupata matibabu na huishia kutumia dawa za asili.

"Tunapopata tatizo la macho tutumie vituo vyetu vya afya na hospitali zetu na kuacha kutumia dawa za asili na dawa za kisuna ikiwemo maji ya chumvi, maji baridi na uzile," alisema mtaalamu huyo wa macho.

Baadhi ya watu waliombukizwa ugonjwa huo, walisema wamepona kwa kusafisha macho kwa kutumia maji ya chumvi ya bahari.

"Mimi na watoto wangu wanne sote tulipata ugonjwa wa macho na tulitumia maji ya bahari kwa muda wa wiki moja tukapona," alisema Asha Khamis, Mkaazi wa Jang'ombe Unguja.

Khadija Bakari, alisema watoto wake wawili walipatwa na ugonjwa huo na kupona baada ya kutibiwa katika kituo cha afya.

ZANZIBAR imeripotiwa kuwa na wagonjwa 4,579 wa macho mekundu ( Red Eyes) ambao wameripotiwa kupatiwa matibabu katika vituo vya afya na hospitalini.

Takwimu hizo zilitolewa juzi na Naibu waziri wa afya Hassan Khamis Hafidh wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu kasi ya maambukizi ya ugonjwa huo visiwani Zanzibar.

# SMZ yagawa vifaranga kwa wafugaji samaki

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi Zanzibar (SMZ) imeanza ugawaji vifaranga wa samaki aina ya mwatiko kwa wafugaji visiwani hapa ili kuongeza uzalishaji na kukuza uchumi wao.

Akizungumza jana baada ya ugawaji wa vifaranga hao katika kituo cha Beit el Ras, Katibu Mkuu Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, Dk. Aboud Suleiman Jumbe, alisema lengo ni Zanzibar kupata samaki kulingana na mahitaji ya wananchi.

Jumbe, alisema katika kuendeleza sekta ya ufugaji, ni vyema wafugaji wapatiwe mafunzo ya kitaalamu kwa kutumia mabwawa na teknolojia mpya.

"Dhamira yetu kuona wizara inaleta mageuzi ya sekta ya ufugaji wa mazao ya baharini ikiwemo samaki aina ya mwatiko na kaa tope na ufugaji wa matango bahari," alisema.

Alisema nchi nyingi zinazoendeleza ufugaji samaki zimeongeza uzalishaji wa kitoweo hicho, hivyo Zanzibar itahakikisha inakuwa miongoni mwao. "Tutatoa ushirikiano wa kina kwa wafugaji wetu na kuwatembelea kuona vifaranga hivi vinakuwa na kutimiza lengo la serikali la kuongeza uzalishaji samaki," alisema.

Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Bahari, Dk. Zakaria Ali Khamis, alisema utafiti wa samaki wa mwatiko, matango bahari na kaa tope umefanyika katika maeneo mbalimbali, hivyo wizara kwa kushirikiana na wataalamu wataendelea na tafiti za maliasili za baharini kuongeza uzalishaji wake Zanzibar.

Mkurugenzi wa Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini, Dk. Salum Sudi Hamed, alisema itahakikisha Zanzibar inakuwa mfano bora kwa uzalishaji wa samaki ili kutosheleza mahitaji.

Mratibu wa Mradi wa Kuendeleza Kilimo na Uvuvi IFAD, Amina Hussein Khamis, alisema katika kuona mradi unaendelea wanaimarisha miundombinu kwa kutoa taaluma ya ufugaji wa samaki kwa wafugaji.

Aliwataka wafugaji kujitokeza kwa wingi kuchukua vifaranga ili kuendelea na ufugaji katika mabwawa yao na kujiongezea kipato. Wafugaji waliopatiwa vifaranga waliishukuru serikali kuwapatia vifaranga na kuwataka wataalamu kuendelea kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara ili waendelee kufuga kwa kutumia teknolojia mpya ya ufugaji.

Siwema Mshenga Issa kutoka Bumbwini Makoba na Ali Juma Kombo, Pwani Mchangani waliwataka wataalamu kuwatembelea ili kujua changamoto wanazokabiliana nazo.

Vifaranga 100,000 vimetolewa kwa vikundi 13 vya wafugaji wa Unguja na vingine vitaendelea kwenye Kisiwa cha Pemba huku asilimia 10 ikibakia kwa uzalishaji katika kituo hicho cha Beit el Ras.

Ofisa Utafiti wa Uvuvi na Mazao ya Baharini, Fatma Suleiman Ali kutoka Idara ya Utafiti wa Uvuvi na Maliasili za Bahari (ZAFIRI), aliwataka wafugaji hao kutumia njia walizoelekezwa kitaalamu ya kuhifadhi vifaranga ndani ya vizimba walivojengewa katika mabwawa ya kufugia baada ya kukabidhiwa kwa usalama wa maisha wao.



Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi akimuapisha Mudrik Ramadhan Soraga kuwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale, Ikulu jijini Zanzibar jana. **PICHA: IKULU**

# Wanawake wafundwa kwa kuhonga mikopo

**Na Mwandishi Wetu,**
ZANZIBAR

WAJASIRIAMALI wanawake wametakiwa kutumia fedha za mikopo kwa malengo waliyokusudia na kurejesha kwa wakati badala ya kuchangia sherehe za harusi na 'kuwahonga' waume zao.

Rai hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Idara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsi na Watoto, Siti Abasi Ali wakati akizungumza na wajasiriamali hao katika Shehia ya Mgambo Wilaya ya Kaskazini 'B' Unguja.

Siti alisema kuwa idadi kubwa ya wanawake wanachukuwa mikopo, lakini hawafikii malengo kutokana na baadhi yao kutumia kuchangia sherehe za harusi na kuwapa waume zao na kushindwa kurejesha kwa wakati.

"Baadhi ya wanaume wakiona unataka kuchukua mkopo wanakuwa na mapenzi ya hali ya juu, lakini mkishanunulia samaki wa tasi wanakimbia, wiki nzima huwaoni na kukuachia mzigo wa deni peke yako." alisema. Aliwataka wajasiriamali hao kumiliki ardhi ili iwasaidie wakatiwa matatizo ikiwemo ya kutengana familia.

Alisema lengo la Rais Dk Samia Suluhu Hassan ni kuhakikisha anawanayanyua wanawake wajasiriamali kiuchumi kwa kupata mikopo isiyokuwa na riba na kuondoka na utegemezi baada ya kuanzisha miradi ya kuwaingizia kipato.

Alisema Serikali inakusudia kujenga vituo maalum vya wajasiriamali wanawake ili wapate sehemu za kukutana, kujadili masuala yao ikiwemo mbinu za kupata fursa zilizopo kupitia mikopo ya Benki ya CRDB ambayo haina riba.

Mkurugenzi huyo, aliwataka wajasiriamali hao kushirikiana, kupendana na kuoneana huruma ili kufikia malengo ya Serikali kuhamasisha wananchi kuanzisha vikundi vya ushirika katika maeneao yao.

"Sio vizuri kusemana kwa wale wenzetu walioshindwa kutoa pesa katika vikundi na badala yake tuangalie mbinu mbadala ya kuweza kuwasaidia kulipa hivyo ninakuombeni wanawake wenzangu tustahimiliane na aibu ya mwanamke mwenzako ni yako," alisema Siti.

Ofisa Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto Wilaya ya Kaskazini 'B', Zuwena Hamad Omar, alisema lengo la kuwakutanisha wajasiriamali hao wanawake ni kubaini changamoto walizonazo katika wilaya hiyo na kuzifikisha sehemu husika ili kutafutiwa ufumbuzi.

Aliwataka wenyeviti, makatibu na washika fedha wa vikundi vya ushirika katika wilaya hiyo kuwaunganisha pamoja wanachama wao ili kufikia malengo ya kuondokana na tatizo la umasikini.

Wajasiriamali hao, walisema wanakabiliwa na changamoto mabalimbali ikiwemo ukosefu wa fedha, masoko, vifungashio na Ofisi za kudumu kwa ajili ya kufanyia kazi na kwa sasa wanatumia Ofisi za kukodi jambo ambalo linapelekea kushindwa kufanya kazi kwa ufanisi.

Patima Makame, miongoni mwa wajasiriamali hao, aliiomba Serikali kupitia kujenga vituo maalumu vya wajasiriamali wanawake kwa ajili ya kukutana na kupanga mikakati na kutatua matatizo ya vikundi vyao.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA PASSPORT YA KUSAFIRIA



**MANDARI MICHAEL NGOWI** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 238383** iliyotolewa makao makuu DAR ES SALAAM PCO mwaka 2019. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/KIN/9837/2024**

## KUPOTEA KWA VYETI




**SALOME LUCAS MATHEW** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye index No. **S0240/0065/2015** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia **ST.JOSEPH SEMINARY MWANZA** mwaka 2015, Cheti cha kuhitimu kidato cha sita chenye index **No. S0216-0666-2018** Kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa Kupitia NGANZA SECONDARY SCHOOL mwaka 2018, Vyeti hivi vimepotea mkoa wa Mwanza. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **PHQ/MWA/MIS/1207/2024.** Taarifa ya Polisi : **PHQ/MWA/MIS/1208/2024**

## PASSPORT IMEPOTEA



**KAMULI MALIGISA MANGWENGU** anatangaza kupotelewa na Passport No. **TAE294505** iliyotolewa mwaka 2019 Dar es Salaam. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu kupitia Kumbukumbu namba: ***PHQ/MWA/NYA/2299/2024.***

## KUPOTEA KWA VYETI



**THOMAS LAZARO MOLLEL** anatangaza kupotelewa na cheti cha kuhitimu kidato cha nne chenye **index No. S0679.0154** Kilichotelewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia KIMANDOLU SECONDARY SCHOOL mwaka 2015, Cheti cha kuhitimu kidato cha sita chenye index No. **S2427/0647** Kilichotolewa na Baraza la mitihani la Taifa Kupitia ISONGOLE SECONDARY SCHOOL mwaka 2018, cheti cha Chuo kilichotelewa na **SOKOINE UNIVERSITY OF AGRICULTURE** Degree level mwaka 2021. Vyeti hivi vimepotea mkoa wa Arusha. Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo cha polisi.
Taarifa ya Polisi: **PHQ/ARU/ARU/529/2024.**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**RAMADHANI MOHAMED MKWAWA** anatangaza kupotea kwa kadi ya gari aina ya **TOYOTA HILUX** yenye usajili namba **T 422 ARL.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **PHQ/DAR/ILA/13028/2024**

**KIBAIGWA AUCTION MART**
**P.O.BOX 20, DODOMA**

## TANGAZO LA MNADA WA HADHARA KIBAIGWA AUCTION MART,

KWA IDHINI NILIYOPEWA NA KAMPUNI YA IMARISHA MAISHA FINANCIAL SERVICES LTD. TUTAUZA MAGARI MANNE,

1. TOYOTA BREVIS NAMBA ZA USAJILI T 215 DRB MALI YA PATRICK ERNEST KALIKUMASO
2. TOYOTA RAV 4 NAMBA ZA USAJILI T 395 DHU MALI YA BARUTI ABBAS JUMA
3. TOYOTA ALPHARD NAMBA ZA USAJLI T 525 CLD MALI YA BAKARI MFAUME KAMBI
4. TOYOTA WISH NAMBA ZA USAJILI T 124 DHP MALI YA ALPHA FILIMON MATANDO. BAADA YA KUSHINDWA KULIPA MKOPO WALIOKOPA. MNADA UTAFANYIKA TAREHE 12/02/2024 MAENEO YA NYERERE SQUARE SAA 10:00 ASUBUHI

**KWA MAWASILIANO ZAIDI PIGA NO. 0688 729841**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**OMARI MZUZA DIWANI** anatangaza kupotea kwa kadi ya pikipiki aina ya **FEKON** yenye usajili namba **MC 988 CNG,** CHASSIS NAMBA: **LDAPAK0B0KGB11769** na ENGINE NAMBA: **162FMJ219F11769.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MKB/RB/181/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**ELIRAMSON PAUL MBISE** Anatangaza kupotelewa kwa kadi ya pikipiki **(HAOJUE)** yenye namba za usajili **MC 887DND,** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilicho karibu nayeye. **PHQ/MOR/MOR/2456/2024**

**IN THE HIGH COURT OF UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**

**MOSHI DISTRICT REGISTRY**
**AT MOSHI**

**LAND APPLICATION NO. 82820 / 2023**

**PAUL FELIX LYIMO..................APPLICANT**

**VERSUS**

**ABRAHAM MLAKI.........................1ST RESPONDENT**
**PAUL ALEX.................................2ND RESPONDENT**

**TO: ABRAHAM MLAKI & PAUL ALEX ,**

**FOR THE DATE OF MENTION,**
**TAKE NOTICE :** That the above case has been fixed for MENTION 15th Day of February 2024 at 09:00 am Before Honourable **A.P KILIMI,J.**
**YOU ARE** required to appear in this Court without fail and you must produce to that day all documents upon which you intend to reply on support of your case.
**GIVEN UNDER MY HAND AND THE SEAL OF THE COURT** this 30th day of NOVEMBER ,2023

DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
MOSHI

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

***Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa***
***Tupigie: +255 - 0677 020701***

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.
TUPIGIE: +255 - 0677 020701
AU
TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI

# Marekani yafikiria ukubwa shambulio la kulipiza kisasi

**WASHINGTON, Marekani**

IKULU ya Marekani imetoa taarifa ya kuwalaumu wanamgambo wanaoungwa mkono na nchi ya Iran kuwa wamefanya shambulio la ndege zisizo na rubani na kusababisha vifo vya askari watatu katika kambi yake moja ya siri iliyoko Jordan.

Msemaji wa Baraza la Usalama la Kitaifa la taifa hillo, John Kirby alisema uchunguzi wa kijasusi unaamini kuwa kundi la Islamic Resistance lenye makazi yake nchini Iraq ndilo lililohusika na shambulio lilotokea Jumapili ya wiki iliyopita.

Juzi, Rais Joe Biden alisema kwamba nchi yake itajibu shambulio hilo kwa nguvu zote, bila ya kufafanua kama ulipizaji kisasi utafanyika lini.

"Maelezo ambayo jumuiya yetu ya ujasusi inaridhika nayo ni kwamba hili lilifanywa na kundi linaloungwa mkono", alisema Kirby katika mkutano na wanahabari.

Kundi la Islamic Resistance la nchini Iraq tayari limedai kuhusika na shambulio huo.

Kirby alirudia kauli kuwa jibu la Marekani litafanyika hatua kwa hatua na kulingana na uchaguzi na ratiba itakayowekwa.

"Kwa sababu hujaona chochote katika saa 48 zilizopita, haimaanishi kwamba hautaona chochote," alisema na kusisitiza "Jambo la kwanza unaweza kuona, lakini haitakuwa jambo la mwisho,"

Rais Biden awali alisema hataki mzozo huo kuwa mpana zaidi katika Mashariki ya Kati, ambako tayari imevurugwa na vita vya Israel katika Ukanda wa Gaza .

Hata hivyo, Iran imekanusha kuhusika na shambulio hilo la ndege zisizo na rubani. Katika hafla iliyofanyika juzi, kamanda wa kikosi cha Revolutionary Guard cha jeshi la Iran, Meja Jenerali Hossein Salami, ambaye ni mshauri wa Kiongozi Mkuu Ayatollah Ali Khamenei, alisema kuwa nchi yake inasikia vitisho vinavyotoka kwa maafisa wa Marekani.

Wakati huo huo, Kundi la Houthi la nchini Yemen lilisema limeishambulia meli ya kibiashara ya Marekani katika bahari ya Shamu.

Katika shambulio hilo jipya, meli iliyohusika ni KOI, ambayo kundi hilo lilisema inamilikiwa na Marekani.

Kampuni ya usalama ya baharini ya Ambrey, ilisema meli hiyo inayofanya kazi kusini mwa bandari ya Aden nchini Yemen, ilikabiliwa na mlipuko.

Hata hivyo, Marekani ilijibu mapigo kwa kufanya mashambulizi ya anga nchini Yemen, yakilenga na kuziharibu ndege 10 zisizo na rubani ambazo zilidaiwa zilikuwa tayari kurushwa.

Kulingana na shirika la habari la Reuters, meli hiyo ya KOI ni maalumu kubeba makontena ambayo inapeperusha bendera ya Liberia, inamilikiwa na kampuni ya Oceonix Services ya nchini Uingereza.

Meli moja ya kampuni inayobeba mafuta inayoitwa Marlin Luanda, iliharibiwa kwa kombora siku ya Jumamosi.

Kundi la Wahouthi wanazichukulia meli zote za Israel, Marekani na Uingereza kama sehemu ya shabaha zao kama kulipiza kisasi kutokana na vita vinavyoendeshwa na Israel dhidi ya wanamgambo wa Hamas katika Ukandaw wa Gaza..

Msemaji wa jeshi la Houthi, Yahya Sarea, alisema kwamba vikosi vya jeshi vya kundi hilo vililenga meli ya wafanyabiashara ya Marekani iitwayo KOI kwa makombora kadhaa ya majini.

**BBC**



Wapiganaji wa kundi la waasi wa M23, linaloendesha shughuli za kijeshi nchini Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo wakiwa kwenye harakati zao. **PICHA: AFP**

# Rais Tshisekedi aikaripia Rwanda

**KINSHASA, DRC**

RAIS wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Felix Tshisekedi amesisitiza kwamba hakuna mazungumzo yoyote yatakayofanyika na nchi ya Rwanda.

Kiongozi huyo alirudia kauli yake hiyo juzi jioni wakati alipokutana na mabalozi wanaowakilisha nchi zao, na kueleza hakutakuwepo kwa majadiliano kuhusu uhuru na mamlaka ya DRC.

Rais Tshisekedi alisema kuwa jeshi la DRC litawasaka maadui mahali popote walipo na bila kujali gharama.

"Serikali inakumbusha haki na wajibu wake wa kuchukua hatua zote muhimu ili kulinda mamlaka na uhuru wa nchi yetu na pia kulinda wananchi pamoja na mali zao. Hakuna mwenye haki ya kuizuia. Kwa hiyo, mimi kama kamanda mkuu wa jeshi letu, nahakikisha tena kwamba tutatumia nguvu zote ili kuondoa vikosi vya Rwanda kwenye eneo letu," alisema Rais Tshisekedi.

Aliishukuru Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC) kwa kupeleka vikosi vyake mkoani Kivu Kaskazini ili kuliunga mkono jeshi lake.

Kwa upande wao, wanadiplomasia walionesha nia yao kuona nchi hiyo ikiinuka na kwa hiyo wataiunga mkono.

Balozi wa Cameroon, Martin Chungong Ayafor, ambaye pia ni mkuu wa mabalozi nchini humo, alitaka wananchi wa taifa hilo kulinda mshikamano na kupiga vita chuki.

"Tunakupongeza kwa kuona haja ya kulinda mshikamano wa kitaifa ukijipa jukumu la kupiga vita chuki, ukabila na mambo mengine yanayopinga maadili. Pia alitoa wito kwa upinzani ukieleza kuwa unayo nafasi yake katika kipindi hiki cha miaka mitano," alisema balozi Ayafor.

# Mwigulu apongeza kampuni kukuza uhusiano

**Na Halfani Chusi**

WAZIRI wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchemba, amesema uhusiano mzuri uliopo kati ya serikali na Kampuni ya Geita Gold Mining Limited (GGML) umechangia kukuza uchumi wa taifa, hususan kwenye makusanyo mazuri ya kodi, ajira na ununuzi wa bidhaa na huduma kutoka ndani ya nchi.

Dk. Mwigulu aliyasema hayo juzi jijini Dodoma alipozungumza na Ofisa Mkuu wa Masuala ya Fedha wa Kampuni ya Uchimbaji Dhahabu ya Anglo Gold Ashanti inayomiliki mgodi huo, Gillian Doran.

Katika mazungumzo hayo, Dk. Mwigulu alisema, "tumekuwa na uhusiano mzuri sana na GGML kama Wizara ya Fedha hususani katika masuala ya kikodi na kiuchumi.

"GGML wamekuwa wadau muhimu sana wa masuala ya kodi na masuala ya kukuza uchumi wa nchi yetu pia wamekuwa uhusiano mzuri na wizara ya kisekta (madini) kwa kuwa moja ya mgodi wa mfano ambao una ushirikiano mkubwa na wizara ya kisekta na wizara nyingine kama sisi," alisema Dk. Mwigulu.

Alisema GGML umekuwa moja ya migodi ya mfano yenye uhusiano mzuri na jamii inayozunguka mgodi kwa kutekeleza ipasavyo Mpango wa Uwajibika wa Kampuni kwa Jamii (CSR).

Pamoja na mambo mambo mengine, alitoa wito kwa kampuni hiyo kutumia viwanda vya kuchenjua dhahabu uliopo nchini ili kuendelea kukuza uchumi wa taifa.

Katika majadiliano hayo, Ofisa Mkuu wa Fedha wa Kampuni ya AngloGold Ashanti (AGA), Gillian Doran aliyemtembelea Dk. Mwigulu akiwa na timu ya uongozi wa kampuni hiyo, alimweleza waziri huyo kuhusu mipango ya muda mrefu ya AngloGold Ashanti kwa Tanzania.

Alimshukuru Dk. Mwigulu kwa kutambua mchango wa GGML ambayo imeendelea kusalia kuwa mlipakodi bora zaidi katika tasnia ya uziduaji nchini.



# WACHEZAJI WA PRISONS WAPIMWA AFYA KUIKABILI YANGA SC LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Tanzania Prisons imeanza kujipanga kuikabili Yanga Februari 11 ambapo wameanza kwa kupima afya wachezaji wake na kuingia kambini kujiandaa na mchezo huo.

Tanzania Prisons itakuwa mwenyeji wa Yanga kwenye mchezo wa Ligi Kuu katika uwanja wa Sokoine jijini Mbeya.

Akizungumza na gazeti hili, Ofisa Habari wa Klabu hiyo, Issaka Chacha amesema kuwa kikosi hicho tayari kimeshaingia kambini na kuanza kufanya mazoezi ya utimamu wa mwili, lakini kabla ya kufanya hivyo wachezaji wote walipimwa afya ili kuweza kuangaliwa kama wanaweza kuhimili aina hiyo ya mazoezi magumu, lakini pia kuanza maandalizi ya mechi za Ligi Kuu.

"Tayari tupo kambini chini ya Kocha Mkuu, Hamadi Hamisi Ally, kabla ya yote wachezaji wetu walikuwa kwenye mapumziko, unajua ligi imesimama kwa muda sasa kupisha Kombe la Mapinduzi na AFCON, sasa waliporudi wachezaji wetu wote waliingia kwenye vipimo, na sisi hatutanii tunapima kweli, sisi ni maafande,"alisema Ofisa Habari huyo mpya ambaye amechukua nafasi ya Jackson Mafulango.

Alizitaja sababu za kuwapima afya wachezaji ambao tayari wamesajiliwa tofauti na klabu zingine ambazo huwapima wakati wa usajili.

"Tumepima afya za wachezaji, kwa sababu walikuwa mapumziko, kwanza tulitaka tujiridhishe je wanaweza kuanza mazoezi ya nguvu?, kwa sababu ligi ilisimama na walikuwa mapumziko isingewezekana kuwafanyisha mazoezi makali bila kuwapima.

Nia ni kujiweka tayari na michezo yetu ya Ligi Kuu tukianza na Yanga," alisema Chacha.

Alisema licha ya kuondokewa na Edwin Balua ambaye ametimkia Simba wamefanya usajili wa wachezaji watano ambao wanaamini wataisaidia timu hiyo.

"Tumewasajili Abdul Karim Segeja, straika aliyetoka Copco, klabu ya Championship, kiungo mzoefu Tariq Simba, kiungo mwingine Ally Msengi, tuna ingizo la Jacob Benedicto kutoka Mbeya Kwanza na Abdallan Mfuko, beki mzoefu sana huyu ameshawahi kuzichezea klabu mbalimbali za Ligi Kuu," alisema.



Bendi ya Jeshi la Polisi ‚Blass Band' ikitumbuiza wakati wa hafla ya siku ya Sheria nchini katika Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Timu 20 zasonga mbele FA Z'bar

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

JUMLA ya timu 20 zimefanikiwa kutinga hatua ya 32 bora na kwenda kuungana na timu za ligi kuu kucheza hatua hiyo baada ya kukamilika kwa hatua ya awali iliyoshirikisha timu 40.

Katika hatua hiyo ya awali ya michuano hiyo ya Shirikisho timu kutoka Ligi daraja la kwanza Kanda ya zile za Mikoa mitatu ya Unguja ambayo ni mkoa wa Mjini Magharibi, Mkoa wa Kaskazini na Kusini Unguja zilishiriki.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa Kamati ya Mashindano ZFF Ali Bakari "Cheupe", alisema hatua ya pili ya michuano hiyo itaanza kutimua vumbi Machi 4 mwaka huu.

Katika hatua hiyo ya pili kutakuwa na timu 32 ambazo zitagawanywa katika makundi mawili, kundi moja likiwa na timu 16 zitakuwa kituo cha Unguja na nyingine zitakuwa kwenye kutuo cha Pemba.

Alisema kamati ya Mashindano ZFF inaendelea na maandalizi ya kuelekea mzunguko huo wa pili hususani katika kupata udhamini utakaochangia kuleta hamasa kubwa ya michuano hiyo.

"Tumemaliza mzunguuko wa kwanza, tunatarajia kucheza mzunguuko wa pili ambao utahusisha pia klabu za Ligi Kuu ya Zanzibar, hatua hii itachezwa kuanzia Machi mpaka 9, baada ya hapo tutatangaza ya hatua inayofuata ya 16 bora" Cheupe.

Aidha akizitaja baadhi ya timu ambazo zimetinga hatua hiyo ya pili kuwa ni Eleven Star, Union Rangers, Villa FC, Nyangobo na Mbweni Academy na Black Lion.

Alizitaja nyingine kuwa Taifa ya Jang'ombe, Inter Zanzibar, Black Sailor, Raskazone, Black Mamba, Polisi, Shangani, Kilimani City, Paje Star, Sharp Boys, Muembe Makumbi City, New King, Negro United na Ujamaa FC.

## 'Serengeti Girls' tayari kuwavaa Zambia

**Na Saada Akida**

KOCHA Mkuu wa timu ya soka ya taifa kwa wasichana wenye umri chini ya maika 18 'Serengeti Girls', Hilda Masanche amesema benchi la ufundi limeridhishwa na utimamu wa mwili wa wachezaji wake na wanachokifanya kwa sasa ni kuwapa mbinu na kuwakumbusha juu ya mikakati ya ushindi waliyoipanga kuelekea mchezo wa kufuzu kombe la Dunia dhidi ya Zambia.

Serengeti Girls wanakibarua kigumu kusaka matokeo chanya katika mchezo huo unaotarajiwa kuchezwa leo nchini humo na baadae wiki ijayo kurudiana katika uwanja wa Azam Complex, Dar es Salaam.

Akizungumza na Nipashe jana, Hilda alisema baada ya kuwasili salama nchini Zambia, wanaendelea na maandalizi na wanafurahi kuona wachezaji wote wapo katika hali nzuri na wanaonyeha kushika kile wanachowafundisha kuelekea kwenye mchezo huo.

Alisema wameangalia zaidi maeneo muhimu na kufanyia kazi kabla ya mchezo huo muhimu.

## Kivumbi Ligi ya Wanawake leo

**Na Saada Akida**

MZUNGUKO wa nane wa Ligi Kuu ya soka ya Wanawake Tanzania Bara inatarajiwa kuendelea leo, wakati viwanja vinne vitakaposhuhudia vumbi la ligi hiyo.

Mabingwa watetezi, JKT Queens watakuwa nyumbani kuwakaribisha Baobab Queens mchezo utakaoanza saa 10:00 jioni.

Kwenye uwanja wa Azam Complex jijini Dar es Salaam, wenyeji Yanga Princess wao watawakaribisha Geita Gold Queens, mchezo huu unatarajiwa kuanza saa 12:00.

Mchezo mwingine unaotarajia kuvuta hisia za mashabiki wengi wa soka la wanawake utashuhudia, Fountain Gate Princess wakiwakaribisha Simba Queens katika dimba la Jamhuri jijini Dodoma, wakati Amani Queens watacheza na Bunda Queens kwenye uwanja wa Ilulu mkoani Lindi na Ceasiaa Queens wataumana na Alliance Girls kwenye uwanja wa Samora, Iringa mechi zote zikitarajiwa kuanza 10:00 jioni.

Kueleke mchezo wao, Kocha Msaidizi wa Simba, Mussa Hassan 'Mgosi', alisema vijana wake wapo tayari kwa ajili ya kusaka alama tatu muhimu dhidi ya wenyeji wao hao.

## ZISIKUPITE

### BROJA AKOMALIWA
KLABU ya Fulham inafikiria kumnunua mshambuliaji wa Chelsea na Albania, Armando Broja mwenye umri wa miaka 22 kwa uhamisho wa dakika za lala salama. **(Evening Standard)**

### GALLAGHER BADO NGUMU
KLABU ya Tottenham Hotspur haina uwezekano wa kufikia bei inayotakiwa na Chelsea ya pauni milioni 50 kumnunua kiungo wa kati wa England, Conor Gallagher na mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23 anatazamiwa kubakia na The Blues hao kwa muda wote uliosalia.**(Talksport)**

### BERGVALL AVUTIA
TOTTENHAM Hotspur inavutiwa na mchezaji wa kimataifa wa Sweden, mwenye umri wa miaka 17, Lucas Bergvall, anayechezea Djurgardens. **(Football London)**

### MOURINHO AITAKA MAN
JOSE Mourinho, ambaye alitimuliwa kama kocha wa AS Roma, anatamani kurejea Manchester United kama kocha wa klabu hiyo ya Old Trafford iwapo nafasi hiyo itatokea. **(Mail)**

### IRAOLA HAONDOKI
KOCHA wa Bournemouth, Andoni Iraola hatarajii mshambuliaji wa England, Dominic Solanke kuondoka katika klabu hiyo Januari, licha ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26 kuhusishwa na Tottenham Hotspur. **(Evening Standard)**

### SOUSA HUYO VILLA
ASTON Villa imekubali dili la kumsaini beki wa pembeni wa England chini ya miaka 19, Lino Sousa kutoka Arsenal. **(Fabrizio Romano)**

### ALBERTO ATAKIWA WOLVES
KLABU ya Wolves ipo kwenye mazungumzo juu ya uhamisho wa mkopo kwa mshambuliaji wa Corinthians na Brazil, Yuri Alberto mwenye umri wa miaka 22. **(Telegraph)**

### GIL KWA MKOPO
KLABU ya Brighton ipo kwenye mazungumzo ya kumleta winga wa Hispania, Bryan Gil mwenye umri wa miaka 22 kwa klabu hiyo kwa mkopo kutoka Tottenham Hotspur. **(Evening Standard)**

### DAHOUD ATAKIWA
KLABU ya Stuttgart inashinikiza kumsajili kiungo wa kati wa Ujerumani, Mahmoud Dahoud mwenye umri wa miaka 28 kutoka Brighton. **(Sky Germany)**

### SOUTTAR AWANIWA
KLABU ya Sheffield United imewasiliana na Leicester City kuhusu uhamisho wa mlinzi wao raia wa Australia, Harry Souttar mwenye umri wa miaka 25, huku wakijaribu kuimarisha safu yao ya ulinzi. **(Football Insider)**

### CORNET ATAKIWA
KLABU ya Crystal Palace inafikiria kumsajili kwa mkopo mshambuliaji wa Ivory Coast mwenye umri wa miaka 27, Maxwel Cornet, ambaye anaweza kuruhusiwa kuondoka West Ham. **(Telegraph)**

## DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# NYOTA WA 5 WANAOWEZA KUTUA KLABU KUBWA ULAYA

**Timu za Ulaya ziko macho kuwafuatilia nyota wanaoonyesha...**

**ABIDJAN, Ivory Coast**

WAKATI Fainali za Mataifa ya Afrika 'AFCON' zikitinga hatua ya robo fainali, vilabu vikubwa barani Ulaya vinafuatilia kwa karibu wachezaji waliofanya vizuri na kuendelea kuonyesha uwezo mkubwa ambapo timu za chini zimeonyesha kiwango kikubwa.

Ni wazi baada ya kumalizika fainali hizo wapo wachezaji ambao wanaweza kusajiliwa na timu mbalimbali, lakini kutokana na viwango vyao wapo wachezaji sita wenye nafasi kubwa ya kusajiliwa na timu kubwa Ulaya.

**Lamine Camara, Senegal**

Lamine Camara nyota wa timu ya taifa ya Ufaransa ambaye timu yake imetolewa hatua ya 16 bora, kwa sasa anakipiga katika klabu ya Metz ya Ufaransa, ni kiungo wa kati ambaye anatajwa kuwa Mwanasoka Bora Chipukizi wa Bara la Afrika mwezi Disemba, Camara mwenye umri wa miaka 20 alionyesha uwezo mkubwa kwa kufunga mabao mawili na kuwa mchezaji bora wa mechi katika ushindi wa Senegal wa mabao 3-0 dhidi ya Gambia.

Camara ameonyesha kiwango kikubwa katika mechi za Senegal na haitashangaza akisajiliwa na klabu kubwa Ulaya.

**Jesus Owono, Equatorial Guinea**

Owono ni kipa wa Alaves ya Hispania, alishinda tuzo ya mchezaji bora wa mechi katika sare ya kwanza ya Equatorial Guinea dhidi ya Nigeria na katika mechi ya ushindi wa 4-0 dhidi ya Ivory Coast.

Owono alicheza bila kufungwa katika mechi tatu kati ya nne za kombe la mataifa ya Afrika 2021.

Owono anaweza kuwa mlinda mlango mkubwa Barani Afrika - akifuata nyayo za magwiji kama Carlos Kameni wa Cameroon,Thomas N'Kono na Vincent Enyeama wa Nigeria.

**Emmam Ashour, Misri**

Ashour, nyota wa Al Ahly na Misri, alikuwa bora katika kutoa usaidizi wa ulinzi na kusonga mbele ili kuongeza mashambulizi ya Misri wakati wa mechi zao za Kundi B.

Licha ya kucheza kwa dakika chache zaidi ya wachezaji wenzake wengi, Ashour bado alimaliza akiwa kileleni kwa kutengeneza nafasi, pasi, pamoja na ubora wa kukokota mpira, haitashangaza akitimkia Ulaya.

**Aboubakary Koita, Mauritania**

Nyota wa Sint-Truiden ya Ubelgiji, alizitimiza ndoto za taifa lake kusonga mbele kwa kutoa mchango mkubwa.

Akiwa na kasi kubwa uwanjanii, kinda huyo mwenye miaka 25 ni winga mwenye jicho la kulenga lango, Mauritania kutinga hatua ya 16 bora, na kujihakikishia ushindi wa kwanza kabisa kwenye michuano hiyo ilipowalaza mabingwa wa Afcon 2019, Algeria bao 1-0.

**Gelson Dala, Angola**

Dala ni mchezaji wa klabu ya Al Wakrah ya Qatar, amefunga mara nne na kuisaidia Angola kufuzu robo fainali kwa mara ya kwanza tangu 2010, na hivyo kumfanya kuwa nyuma kwa bao dhidi ya kinara wa mabao Emilio Nsue.

Baada ya mabao mawili dhidi ya Mauritania katika hatua ya makundi, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 27 alifunga mabao mengine mawili yaliyosaidia Angola kutinga robo

# GUARDIOLA ASIFU KIWANGO CHA ALVAREZ

**MANCHESTER, England**

PEP Guardiola amesifia uchezaji "wa kuvutia " wa Julian Alvarez baada ya mabao mawili ya mshambuliaji huyo kusaidia ushindi wa 3-1 wa Manchester City dhidi ya Burnley, juzi.

Alvarez, akisherehekea kutimiza umri wa miaka 24 ya kuzaliwa kwake, alifunga mabao mawili katika kipindi cha kwanza kabla ya bao la Rodri kuhitimisha ushindi wa nane mfululizo kwa mabingwa hao wa Ulaya.

Ameen Al-Dakhil alifunga bao la kufutia machozi dakika za mwisho kwa wageni ambalo halikuweza kufuta tabasamu ya Guardiola.

Aliiambia TNT Sports: "Haikuwa rahisi kwetu, lakini tulikuwa wanyenyekevu vya kutosha kucheza jinsi unavyopaswa kucheza.

"Ni pointi tatu zaidi, yeye (Alvarez) ni mchezaji wa aina yake. Nimefurahishwa sana na sio tu mabao yake lakini kwa mambo mengi, mengi anayofanya. Nzuri sana," alisema Guardiola.

Erling Haaland alirejea kutoka kwenye majeraha kama mchezaji wa akiba kipindi cha pili, huku Kevin De Bruyne alianza mchezo kwa mara ya kwanza tangu mechi ya mabadiliko ya wikiendi ya ufunguzi wa msimu.

Mbelgiji huyo alikuwa mpishi wa bao la pili la Alvarez na Guardiola akafurahishwa na uchezaji wake.

Bosi huyo raia wa Hispania alisema: "Tulimwona (De Bruyne) akiwa na mdundo mzuri sana.

"Alikuwa mzuri sana. Lazima tuchukue mchezo mmoja kwa wakati mmoja sasa, tunapofanya vizuri siku za nyuma imekuwa ni kwa sababu tulifikiria mechi inayofuata.

"Sijui nini kitatokea. Tutapoteza pointi lakini natumaini sio nyingi.

"Sasa tunajiandaa kwa Brentford. Msimu uliopita hatukuweza kushinda pointi moja dhidi yao."



# Klopp: Nunez alihuzunika kugonga nguzo mara nne

**LIVERPOOL, England**

Kocha Jurgen Klopp amemwita nyota wake Darwin Nunez kuwa ni "mwenye bahati mbaya" baada ya fowadi huyo wa Liverpool kugonga nguzo ya goli mara nne na kushindwa kufunga wakati wa ushindi wa 4-1 kwenye mchezo wa Ligi Kuu ya England dhidi ya Chelsea, juzi.

Liverpool wamedumisha uongozi wao wa pointi tano dhidi ya wapinzani wao wa karibu Manchester City na Arsenal kufuatia mabao ya Diogo Jota, Conor Bradley, Dominik Szoboszlai na Luis Díaz na Christopher Nkunku akiifungia Chelsea.

Lakini ingawa Núñez alimaliza mchezo kwa kutoa pasi ya bao kwa Diaz, Klopp alisema mchezaji huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 85 kutoka Benfica alikuwa "amefadhaika" baada ya kukosa nafasi nyingi.

"Núñez]alikuwa na kipindi cha kwanza cha kichaa, kisichowezekana kutetea, kizuri sana," alisema Klopp katika mkutano wake na waandishi wa habari baada ya mechi.

"Ni mara ya kwanza tangu tuhesabu kwamba mchezaji aligonga nguzo ya goli mara nne kwenye mchezo na akakosa penalti.

"Alisikitishwa sana na yeye mwenyewe kukosa penalti, lakini ni wachache. Ilikuwa ngumu sana kwake. Unaweza kuona wakati wa mapumziko kwamba alijichukia, alikosa bao la kichwa pia kipindi cha pili, lakini akatengeneza bao.

"Ni kichaa linapokuja suala la kufunga, sisi tulifunga mabao manne, kwa hiyo nani anajali yale ambayo hakufunga, atafunga, yatakuja, ana umbo la hali ya juu, alikuwa na bahati mbaya."

Liverpool itasafiri kwenda Arsenal Jumapili kwa mchezo muhimu katika mbio za ubingwa, na Klopp alisema pambano hilo ni "kubwa."

"Mchezo unaofuata unakuja baada ya siku nne, jambo ambalo sikufikiri lingewezekana," alisema.

"Lakini mchezo unaofuata ni mkubwa. Arsenal. Hebu tupone na twende tena."

# Ten Hag aeleza sababu kumsamehe Rashford

**MANCHESTER, England**

ERIK ten Hag amesema adhabu zilizotolewa kwa Marcus Rashford na Jadon Sancho zilikuwa tofauti kwa sababu "Jadon alichagua kutangaza hadharani."

Rashford jana alikuwepo kwa mechi ya Ligi Kuu ya Manchester United dhidi ya Wolves baada ya mazungumzo ya wazi na Ten Hag Jumatatu kufuatia mshambuliaji huyo kujirusha kwenye klabu ya usiku huku akidai ni mgongwa.

Sancho, kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu yake ya zamani ya Borussia Dortmund baada ya kuhoji hadharani sababu za Ten Hag kumuondoa kwenye kikosi kwa ajili ya mchezo dhidi ya Arsenal, Septemba mwaka jana.

Sancho alilazimika kufanya mazoezi peke yake kwa zaidi ya miezi minne huku Rashford akifanya mazoezi ya kawaida na wachezaji wenzake siku ya Jumatatu na Ten Hag amesema mbinu tofauti zilitokana na chapisho la Sancho ambalo sasa limefutwa kwenye mtandano wa X, zamani Twitter.

"Tunaweza kutatua kila kitu ndani. Jadon alichagua kujitokeza hadharani," alisema Ten Hag.

Rashford aliingia matatani baada ya kuiripoti kuwa mgonjwa sana na hawezi kufanya mazoezi siku ya Ijumaa, lakini usiku wake akapigwa picha akiwa kwenye klabu ya usiku ya Belfast akila bata.

Pia alikosa mazoezi siku ya Jumamosi na hakuwepo kwenye ushindi wa 4-2 dhidi ya Newport County katika Kombe la FA Jumapili.

"Kwanza kabisa, wachezaji katika kiwango hiki wanahitaji kujisimamia wenyewe, hilo ndilo unaloweza kudai kutoka kwa mchezaji," alisema Ten Hag kwenye mkutano na waandishi wa habari.

"Mchezaji lazima ajue ni kipi kizuri na kipi si kizuri. Unapotaka kucheza soka ya hali ya juu, inataka mfumo fulani wa maisha."

Rashford na Sancho hawako peke yao katika kuasi sheria kali za Ten Hag.

Mholanzi huyo pia alitofautiana na Cristiano Ronaldo kabla ya kuhamia Al Nassr na amemwadhibu kijana wa Argentina, Alejandro Garnacho.

HABARI MICHEZO

# SIMBA WAWAGEUKIA MASHUJAA,TABORA

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kutinga hatua ya 16 bora ya kombe la Shirikisho (FA), Kocha Msaidizi wa Simba, Seleman Matola ameweka wazi kuwa akili yao yote sasa wanawaza mechi mbili za ugenini za Ligi Kuu Tanzania Bara watakazocheza ndani ya siku nne.

Kikosi cha Simba kimeondoka jana asubuhi kuelekea Kigoma tayari kwa ajili ya mchezo wa kiporo dhidi ya wenyeji wao Mashujaa FC utakaochezwa kesho uwanja wa Lake Tanganyika, baada ya mchezo huo wataanza safari kuelekea Tabora kucheza na Tabora United mchezo uliopangwa kuchezwa Februari 6 kwenye uwanja wa Alli Hassan Mwinyi.

Simba juzi ilifanikiwa kushinda mechi ya hatua ya 32 kwa kuifunga Tembo FC ya mkoani Tabora kwa mabao 4-0 kwenye mchezo uliochezwa Azam Complex, Chamazi.

Matola, alisema mchezo huo haukuwa rahisi lakini wameridhishwa na matokeo na namna wachezaji walivyocheza.

"Mechi yetu inayofuata dhidi ya Mashujaa FC ni mechi ngumu na uwanja wake mgumu lakini tumejipanga kwa ajili ya kupata ushindi. Wachezaji wapya wameanza vizuri kama tulivyowaona kwenye mchezo wa jana (juzi) na Tembo FC, lakini wanatakiwa kupata muda wa kuzoea mazingira na kuzoeana na waliowakuta," alisema Matola.

Wakati huo huo, Mshambuliaji mpya wa Simba , Pa Omar Jobe ambaye alifumga bao katika mechi yake ya kwanza tangu amesajiliwa kipindi cha dirisha dogo, alisema amekuja kufanya kazi na sio vinginevyo.

Jobe, alisema amekuja Tanzania kufanya kazio na kuipa mafanikio timu yake mpya na hajaja Tanzania kwa ajili ya mapumziko.

"Najua Simba timu kubwa, na michuano ya CAF nimewahi kucheza sio mgeni katika mashindano hayo, nitahakikisha nawapa furaha mashabiki kwa kufanya vizuri kwenye timu," alisema Jobe.




Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano wa Sportpesa, Sabrina Msuya (kushoto) akiwa na Meneja wa Wateja wakubwa wa M-Pesa, Amina Said (katikati) baada ya kutangaza ushirikiano wa makampuni hayo kutoa huduma mpya ya ubashiri michezo. **PICHA: SPORTPESA**

# Sportpesa,Vodacom waleta kitu kipya

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Sportpesa imeungana na Vodacom kuwapa wateja wao bidhaa mpya ya Supa Jackpot kupitia huduma ya M Pesa.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Sportpesa, ushirikiano huo unalenga kuwapa wateja nafasi ya kujishindia Jackpot na kubadili maisha yao, kuburudika huku wakifuatilia mechi za mpira wa miguu na kubashiri michezo waipendayo kila wiki.

Katika taarifa hiyo, Mkuu wa Idara ya Uhusiano na Mawasiliano, Sabrina Msuya, alisema kupitia Supa Jackpot mchezaji anaweza kujishindia bonasi mpaka Shilingi Bilioni moja endapo atabashiri kwa usahihi mechi kuanzia 12 mpaka 16 kwenye Jackpot iliyopo kwenye menyu ya M-Pesa.

"Kila wiki tutakuwa tukitangaza washindi wa bonasi na tunamatumaini makubwa kupata mshindi wa bilioni moja kutoka Vodacom," alisema Sabrina.

Kwa upande wake, Meneja wa wateja wakubwa wa M Pesa, Amina Said, amelisisitiza wateja kushiriki katika Supa Jackpot kuweza kushinda mamilioni ya fedha.

Alisema kila kitu kimewekwa kwenye menyu ya huduma hiyo ambapo wateja na mashabiki wa mpira wanaotaka kubashiri wanatakiwa kuingia kwenye menyu hiyo.

## Rekodi yaibebea Yanga kwa Kagera

INATOKA UK. 24

Hiyo inaonyesha Yanga ina safu bora ya ulinzi ikiwa chini ya kipa Diarra na mabeki wake Joyce Lomalisa, Yao Kouassi Ibrahim Bacca , Dickson Job na Bakari Mwamnyeto

Kukosekana kwa Diarra leo kunaweza kumpa nafasi kipa Aboutwaleeb Mshery ambaye alidaka mechi iliyopita ya kombe la shirikisho la Azam (ASFC) dhidi ya Hausung ambayo Yanga ilishinda mabao 5-1.

Pia Yanga leo inaweza kumtumia mshambuliaji wao mpya raia wa Ivory Coast Joseph Guede ambaye alitambulishwa juzi kwenye mechi ya ASFC.

Kwa upande wa Kagera Sugar wenyewe hawakuwa nyuma kujiimarisha kwenye dirisha dogo la usajili ili kujinasua katika nafasi ya 14 waliyopo sasa kwenye msimamo wa ligi.

Timu hiyo imemsajili mshambuliaji Mcameroon Mbaraka Amza kutoka Coast Union na leo anaweza akaanza dhidi ya Yanga akishirikiana na nyota wengine kama Obrey Chirwa, Mbaraka Yusuph na Degratius Mafie.

Kocha wa Kagera Sugar, Fred Felix Minziro alisema mechi dhidi ya Yanga inamuumiza kichwa lakini wako tayari kupambana nao kuhakikisha wanapata ushindi.

Minziro ameanza kukinoa kikosi hicho mapema wiki hii akichukua mikoba ya Meck Maxime ambaye ametimkia Ihefu.

"Kikosi chetu kina mchanganyiko wa wazoefu na damu changa hivyo ni jambo zuri kwetu kuhakikisha tunapambana katika michezo yetu ijayo ukiwemo dhidi ya Yanga.

"Ni jambo gumu, nimefika tu kwenye hii timu nakutana na Yanga, sio jambo rahisi kabisa na naumiza kichwa kwani wapinzani wetu ni timu bora lakini tuombe Mungu ndiye anapanga kila kitu,na tuko tayari kwa mapambano " alisema Minziro.

## Kivumbi cha robo fainali AFCON

INATOKA UK. 24

mosi kwenye Uwanja wa Paix kule mjini Bouake.

**Cape Verde v Afrika Kusini**

Cape Verde haijashindwa, itacheza na Afrika Kusini ambao waliiondoa Morocco katika hatua ya 16 bora.

Cape Verde wamekuwa na mwendo mzuri katika kipindi chote cha mashindano tofauti na Afrika Kusini ambao wamekuwa wakitofautiana na matokeo.

Kocha wa Afrika Kusini, Hugo Broos atawategemea Evidence Makgopa, Percy Tau na Themba Zwane dhidi ya Cape Verde.

Ingawa ni ngumu lakini Cape Verde wameona yote dhidi ya nchi zenye uzoefu na wamefanikiwa.

Mchezo huu utafanyika kesho kwenye Uwanja wa Charles Konan Banny mjini Yamoussoukro.

Michezo
Ijumaa Februari 2, 2024
Nipashe

Guardiola asifu kiwango cha Alvarez UKURASA 22





Djigui Diarra (Mali)          Henock Inonga (Congo)

# KIVUMBI CHA ROBO FAINALI AFCON LEO

## Vita ya kusaka tiketi ya kutinga hatua ya nusu fainali inaanza ambapo....

**ABIDJAN, Ivory Coast**

ROBO fainali ya michuano ya kombe la mataifa ya Afrika, AFCON, inatazamiwa kuwa na mechi za kuvutia katika miji mitatu kuanzia leo Ijumaa.

Hatua ya 16 bora ilitoa michezo ya kusisimua pamoja na mshtuko na baadhi ya waliotabiriwa kufanya vizuri walishia kuondoka kwenye fainali hizo wakiwemo mabingwa watetezi Senegal na wana nusu na washindi wa nne fainali ya Kombe la Dunia la 2022, Morocco.

Hatua hiyo ya robo fainali inawashuhudia wachezaji wawili pekee wanaocheza Ligi Kuu Tanzania Bara, Henock Inonga wa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo na Djigui Diarra wa mali ambao watakuwa na kazi ya kuzisaidia timu zao kutinga nusu fainali.

Hapa kuna michezo ya kuzingatia katika robo fainali na jinsi mambo yanavyotarajiwa kuwa.

**Nigeria v Angola**

Super Eagles watamenyana na Angola katika robo fainali ya kwanza leo Ijumaa, katika uwanja maarufu wa Felix Houphouet-Boigny.

Angola watakuwa na matumaini ya kuendeleza hadithi yao tamu dhidi ya timu mojawapo inayopewa nafasi kubwa ya kuibuka mabingwa wa mashindano hayo, Nigeria.

Kikosi cha ulinzi thabiti cha Nigeria kikiwa na William Troost - Ekong, Calvin Bassey na Semi Ajayi kitajaribiwa na fowadi wa Angola, Jacinto Dala, Gilberto na Mabululu katika mchezo huu unaotarajiwa kuwa na mvuto.

**Congo v Guinea**

Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo ambao bado hawajashinda mchezo wowote kwenye kinyang'anyiro hicho watakuwa na Guinea kukabiliana nao katika hatua ya robo fainali.

Mohamed Bayo mara mbili amekuwa mwokozi wa Guinea katika michuano hii, akifunga dhidi ya Cameroon na kuwasaidia kupata pointi moja na alifunga bao dhidi ya Equatorial Guinea katika hatua ya 16 bora.

Huku mafanikio ya CHAN ya 2009 nchini Ivory Coast yakitarajiwa kuwa chachu, D.R Congo itatoa kila kitu dhidi ya Guinea.

Mchezo utachezwa leo Ijumaa katika uwanja wa Olympique Alassane Ouattara mjini Abidjan.

**Mali v Ivory Coast**

Wenyeji walifanya vyema na kuwaondoa mabingwa watetezi, Senegal kwa mikwaju ya penalti katika hatua ya 16 bora.

Hii ilifuatia mwisho mbaya wa kampeni yao ya hatua ya makundi ambapo walipoteza kwa Nigeria na Equatorial Guinea na kusonga mbele kwa kufungwa mabao 5 wakisonga mbele kwa mlango wa 'Best Looser'.

Ivory Coast wameshindwa kufunga bao ndani ya dakika tisini ya mchezo katika michezo yao mitatu iliyopita na wanatarajia kufanya marekebisho kwa kurejea kwa Sebastien Haller pale mbele.

Mali licha ya kutocheza vizuri katika hatua ya makundi ilifanya vyema dhidi ya Burkina Faso katika hatua ya 16 bora.

Mchezo huu utafanyika kesho Juma-

INAENDELEA UK. 23

# Rekodi yaibebea Yanga kwa Kagera Sugar

**Na Oliver Albert**

WAKATI mabingwa watetezi, Yanga leo wakiwa ugenini kucheza na Kagera Sugar kwenye mchezo wa Ligi Kuu. rekodi zinawabeba wababe hao dhidi ya Kagera Sugar.

Timu hizo zinaumana leo kwenye uwanja wa Kaitaba mjini Bukoba ukiwa ni mchezo wa kwanza wa Ligi Kuu tangu kusimama kwa muda kupisha michuano ya Kombe la mapinduzi na AFCON.

Mchezo huo wa kiporo unawakutanisha Yanga ambayo itakosa huduma ya wachezaji wake muhimu,Stephano Aziz Ki, kipa Djigui Diarra ambao wapo katika majukumu ya timu zao taifa pamoja na mshambuliaji Agustine Okra na mabeki Bakari Mwamnyeto na Ibrahim Bacca ambao nao wataukosa mchezo huo kwa sababu tofauti tofauti.

Diarra ambaye aliingoza Mali kutinga robo fainali ya michuano ya AFCON kwa kuichapa Burknafaso mabao 2-1 ambayo anaichezea mchezaji mwenzake wa Yanga Stephano Aziz Ki.

Yanga itaingia katika mchezo wa leo ikijivunia rekodi bora kila inapocheza ugenini dhidi ya Kagera Sugar tangu mwaka 2015.

Kwa miaka tisa mfululizo tangu mwaka 2015, Kagera Sugar haijawahi kuifunga Yanga kwenye uwanja wao wa nyumbani iwe inacheza Kaitaba au CCM kirumba na mara zote walipokutana 'Wanankurukumbi' hao wamekuwa wakiambulia vipigo.

Katika mechi nane walizokutana waakiwa nyumbani kwa miaka tisa mfululizo, zote Kagera Sugar imepoteza dhidi ya Yanga hivyo kuonyesha kuwa inatakiwa kuwa makini hata katika mchezo wa leo.

Mara ya mwisho Kagera kuifunga Yanga kwenye uwanja wa Kaitaba ilikuwa Novemba Mosi mwaka 2014 iliposhinda bao 1-0, bao lililofungwa na Paul Ngway.

Ushindi mkubwa ambao Yanga imewahi kupata ilipocheza na Kagera Sugar kwenye uwanja wa Kaitaba ni ule wa mabao 6-2 Oktoba 16 mwaka 2022.

Timu zote zinaingia kwenye mchezo wa leo zikiwa na rekodi tofauti, Yanga ikiwa ndio timu pekee ambayo imeruhusu mabao machache kwenye Ligi Kuu Bara, ikiwa imefungwa mabao sita tu wakati Kagera Sugar ndio timu pekee kwenye ligi ambayo imefunga mabao machache zaidi ( nane).

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002